**UCHUNGUZI WA MIGONGANO YA KIMBARI KATIKA MUKTADHA WA ZANZIBAR YA UBAADAUKOLONI: UCHANGANUZI WA RIWAYA YA *VUTA N'KUVUTE* NA *MUNGU HAKOPESHWI***

**ULFAT ABDULAZIZ IBRAHIM**

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SHARTI PEKEE LA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UMAHIRI YA KISWAHILI (M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA KATIKA IDARA YA LUGHA NA TAALUMA ZA FASIHI**

**2023**

**UTHIBITISHO**

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma tasinifu hii inayohusu '***Uchunguzi wa Migongano ya Kimbari katika Muktadha wa Zanzibar ya Ubaadaukoloni: Uchanganuzi wa Riwaya ya Vuta N'kuvute na Mungu Hakopeshwi',*** na kuipendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kutunukiwa shahada ya Umahiri (M.A) ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

______________________________

Dkt. Mohamed Omary Maguo

(Msimamizi)

Tarehe______________________

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili sehemu yoyote ile ya tasnifu hii kwa njia yoyote ile kama vile, kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba.

## TAMKO

Mimi, Ulfat Abdulaziz Ibrahim, ninakiri kuwa tasinifu hii inayohusu ‘**Uchunguzi wa Migongano ya Kimbari katika Muktadha wa Zanzibar ya Ubaadaukoloni: Uchanganuzi wa Riwaya ya *Vuta N’kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*’,** ni kazi yangu mwenyewe. Haijatolewa na haitatolewa kwa mahitaji ya kutunukiwa shahada ya Uzamili au shahada nyingine yoyote katika Chuo Kikuu kingine chochote.

Saini_____________________________

Tarehe_________________________

## TABARUKU

Napenda kuitabaruku kazi hii kwa wazazi wangu, familia na walimu wangu walionisomesha tokea elimu ya awali mpaka hapa nilipofikia.

## SHUKURANI

Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai, uzima, nguvu na fahamu katika kipindi chote cha masomo yangu. Pili, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa msimamizi wangu kwa kuniongoza vyema katika kila hatua ya utafiti huu, pamoja na walimu wengine kwa msaada walionipatia katika kipindi chote cha masomo yangu. Tatu, shukurani za pekee ziwaendee wazazi na familia yangu kwa ujumla kwa kuwa nami bega kwa bega katika kufanikisha masomo yangu asanteni.

## IKISIRI

Tasinifu hii inahusu '**Uchunguzi wa Migongano ya Kimbari katika Muktadha wa Zanzibar ya Ubaadaukoloni: Uchanganuzi wa Riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*',** Ili kutimiza kusudi hilo kulikuwa na malengo mahsusi matatu. Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha makundi ya kimbari yanayoonekana katika jamii ya Zanzibar ya Baadaukoloni kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*, lengo la pili lilikuwa kuchanganua aina za migongano ya kimbari ya jamii ya Wazanzibari wa Baadaukoloni kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi* na lengo la tatu lilikuwa kutathmini mikakati ya utangamano wa kimbari inayopendekezwa katika riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi.* Data za msingi zilikusanywa kwa mbinu ya usomaji makini na uchambuzi wa kinyaraka. Mjadala na uchambuzi wa data uliongozwa na nadharia ya Ubaadaukoloni. Matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba katika riwaya teule kuna makundi ya kimbari ya kundi la Waafrika au Waswahili, kundi la Waarabu, kundi la Wahindi na kundi la Machotara. Kwa upande wa aina za migogoro ya Kimbari tumebaini aina mbili ambazo ni hisia-kinzani katika utambulisho na hisia-kinzani katika ndoa na mapenzi. Matokeo ya utafiti yanaendelea kuonesha kwamba mikakati ya kuondoa migongano hiyo ni kufanya mabadiliko ya tabia na utambulisho mpya wa Wanajamii kuwa na mapenzi yasiyokuwa na mipaka ya kimbari na uvunjaji wa mila za kinasaba. Utafiti huu unapendekeza utafiti zaidi katika eneo hili la umbari na fasihi ufanyike zaidi na pia kutoa elimu kwa umma juu ya watu wote kuishi kwa pamoja na kushirikiana katika mambo ya kijamii kutasaidia katika kupunguza na hata kuondoa migongano ya kimbari.

# YALIYOMO

UTHIBITISHO .......... ii

HAKIMILIKI .......... iii

TAMKO .......... iv

TABARUKU .......... v

SHUKURANI .......... vi

IKISIRI.. .......... vii

YALIYOMO .......... viii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .......... 1**

1.1 Utangulizi .......... 1

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti .......... 1

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti .......... 7

1.4 Lengo Kuu la Utafiti .......... 7

1.4.1 Malengo Mahsusi .......... 7

1.4.2 Maswali ya Utafiti .......... 8

1.5 Umuhimu wa Utafiti .......... 8

1.6 Mawanda ya Utafiti .......... 9

1.7 Mpangilio wa Tasinifu .......... 9

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA .......... 10**

2.1 Utangulizi .......... 10

2.2 Muhtasari wa Riwaya ya Vuta N'kuvute .......... 10

2.3 Muhtasari wa Riwaya ya Mungu Hakopeshwi .......... 12

2.4 Zanzibar ya Wakati wa Ukoloni na Ubaadaukoloni .................................... 14
2.5 Masuala ya Kimbari kwa ujumla ................................................................ 19
2.6 Kiunzi cha Nadharia ya Ubaadakoloni ....................................................... 24
2.7 Namna Dhana za Homi Bhabha Zilivyotumika katika Utafiti Huu ............. 27
2.7.1 Uchotara ................................................................................................... 27
2.7.2 Hisia-Kinzani ............................................................................................ 28
2.7.3 Uwanda-Mpito ........................................................................................... 29
2.8 Muhtasari ..................................................................................................... 30

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........................................................... 32**

3.1 Utangulizi ..................................................................................................... 32
3.2 Eneo la Utafiti .............................................................................................. 32
3.3 Usanifu wa Utafiti ........................................................................................ 32
3.4 Vyanzo vya Data za Utafiti ........................................................................... 33
3.5 Uteuzi wa Watafitiwa ..................................................................................... 33
3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ...................................................................... 33
3.6.1 Mbinu ya Usomaji Makini ............................................................................ 34
3.7 Uchambuzi wa Data ........................................................................................ 34
3.8 Usahihi na Ubora wa Data .............................................................................. 35
3.9 Maadili ya Utafiti ............................................................................................ 35
3.10 Hitimisho ....................................................................................................... 36

**SURA YA NNE: KUBAINISHA MAKUNDI YA KIMBARI KATIKA JAMII YA ZANZIBAR YA BAADAUKOLONI KUPITIA RIWAYA YA VUTA N'KUVUTE NA MUNGU HAKOPESHWI .......... 37**

4.1 Utangulizi ........ 37

4.2 Makundi ya Kimbari Yenye Migongano katika Jamii ya Wazanzibari ....... 37

4.2.1 Kundi la Waafrika au Waswahili ........ 38

4.2.2 Kundi la Waarabu ........ 40

4.2.3 Kundi la Wahindi ........ 41

4.2.4 Kundi la Machotara ........ 42

4.2.4.1 Uchotara wa Kiutamaduni ........ 44

4.2.4.2 Uchotara wa Kimbari ........ 46

4.3 Hitimisho ........ 49

**SURA YA TANO: KUCHANGANUA AINA ZA MIGONGANO YA KIMBARI YA JAMII YA WAZANZIBARI WA BAADAUKOLONI KATIKA RIWAYA YA VUTA N'KUVUTE NA MUNGU HAKOPESHWI ........ 50**

5.1 Utangulizi ........ 50

5.2 Hisia-Kinzani katika Utambulisho ........ 51

5.3 Hisia-Kinzani katika Ndoa na Mapenzi ........ 55

5.4 Hitimisho ........ 58

**SURA YA SITA: MIKAKATI YA KULETA UTANGAMANO WA KIMBARI INAYOPENDEKEZWA NA WAANDISHI KATIKA RIWAYA ZA VUTA N'KUVUTE NA MUNGU HAKOPESHWI ........ 60**

6.1 Utangulizi ........ 60

6.2 Mabadiliko ya Tabia na Utambulisho Mpya wa Wanajamii ........ 60

6.3 Mapenzi Yasiyo na Mpaka wa Kimbari ........ 67

6.4 Uvunjaji wa Mila za Ndoa za Kinasaba ........ 71

6.5 Hitimisho ........ 75

**SURA YA SABA: MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO ........ 76**

7.1 Utangulizi ........ 76

7.2 Utoshelevu wa Nadharia ........ 76

7.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ........ 76

7.4 Mchango wa Utafiti ........ 78

7.5 Mapendekezo ........ 78

7.6 Hitimisho ........ 79

**MAREJELEO…… ........ 80**

**VIAMBATANISHO ........ 88**

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Ubaadaukoloni ni dhana inayorejelea kipindi ambacho mataifa yaliyokuwa yakitawaliwa na wakoloni yamekuwa huru na kujitawala wenyewe. Vilevile dhana hii inaakisi mtazamo unaotumiwa na wahakiki mbalimbali ambao wanasawiri kuchambua na kukosoa hali ya mambo katika nchi zilizokuwa Makoloni ya Ulaya hadi miaka ya karibuni, hususani katika nchi za Afrika, Asia na Karibiani.

Utafiti huu unahusu 'Migongano ya kimbari katika muktadha wa Zanzibar ya Ubaadaukoloni: Uchanganuzi wa *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*. Sura hii ya kwanza ni ya utangulizi inayofafanua masuala mbalimbali ya kiutangulizi kuhusiana na utafiti wetu. Masuala yanayofafanuliwa katika sura hii yanahusu usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti  na mpangilio wa tasnifu.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Tafiti zihusuzo migongano ya kiutambulisho katika kazi za fasihi za Kiubaadaukuloni zinajitokeza kwa wingi katika jamii ambazo zina historia ya kujengwa na uchotara na mwingiliano mbalimbali ambao mara nyingi husababisha masuala ya migongano ya kiutambulisho kuwa sehemu yake ya changamoto za kiutamaduni, kisiasa, kiuchumi na kijamii (Dizayi, 2015; O'Reilly, 2001 & Sheriff, 2001).

Kipindi cha Kibaadaukoloni ni wakati ambapo makoloni yamefanikiwa kupata uhuru wake kutoka kwa Wakoloni hususani wa Ulaya. Kwa mujibu wa Mulokozi (2017)

Ubaadaukoloni ni mtazamo unaosawiri kuchambua na kukosoa hali ya mambo katika nchi zilizokuwa Makoloni ya Ulaya hadi miaka ya karibuni, hususani katika nchi za Afrika, Asia na Karibiani. Anabainisha kuwa nchi hizo ingawa ziko huru, bado zinakabiliwa na migongano na mtanzuko wa kiutamaduni na utambulisho wake. Baada ya kuanguka kwa himaya ya Kikoloni, matokeo huwa ni kuacha athari ya kimtanzuko kitaifa na kimbari kwa watawaliwa. Hali hii inatokana na ukweli kwamba Ukoloni si utawala wa kiuchumi pekee, bali ni utawala wa kitamaduni ambapo watawaliwa huwa bado wanafungamana nao (Ashcroft, 1994).

Moja ya matokeo au athari ya Ubaadaukoloni katika jamii ni kuwepo kwa migogoro au migongano ya kimbari. Mbari ni jamii ya watu wa kitovu kimoja, ukoo, kabila au jamii yenye utamaduni mahsusi (TUKI, 1981:229). Watu hao au kikundi hicho hujitambua kuwa ni wa asili moja kiuzazi, kilugha, kihistoria na kijamii. Matabaka ya kimbari wakati wa Ubaadaukoloni yana sifa kadhaa, ikiwemo kugombana kwa wanajamii wa mbari mbalimbali kuwa na haki sawa nyakati za kipindi cha baada ya uhuru. Pamoja na mambo mengine, ukoloni ni miongoni mwa vitu vilivyowajengea wananchi wa jamii ya Wazanibari misingi ya matabaka mbalimbali ya kimbari. Wakoloni hasa Waingereza, waliendeleza mfumo wa matabaka na ubaguzi wa kimbari katika makoloni yao na hawakujishughulisha na kuleta utangamano baina ya makundi ya kimbari (Dizayi, 2015). Hivyo, suala la utambulisho ni suala mtambuka katika kipindi cha Ubaadaukoloni na katika fasihi ya wakati huu na inaweza kuchukuliwa kuwa ni mgogoro unaojitokeza katika jamii mbalimbali za Ubaadaukoloni.

Suala la utambulisho katika jamii ya Zanzibar ni tata. Pamoja na kuwepo kwa wanajamii wenye mbari mahsusi, pia wapo machotara wanaonasibishwa na Uarabu na Uhindi ambao wanahistoria ndefu ya kuingiliana na wenyeji tangu karne ya 10 katika ukanda huu wa Afrika ya Mashariki. Ukanda wa Afrika ya Mashariki, hususani Zanzibar, umekuwa ni sehemu ya makusanyiko ya Waafrika, Washirazi, Waarabu, Wahindi na tamaduni za Kiulaya kwa karibu Milenia mbili kiasi cha kulifanya eneo hilo liwe chachu ya kuibua masuala ya kidini, kimbari, rangi, matabaka na siasa katika Afrika ya Mashariki.

Kuanzia mwaka 1000 B. K, kikundi cha kwanza cha wazawa kilipoanza kufika pande hizi za Afrika, walikuja baadaye kuchanganyika na Waarabu, Washirazi na wafanyabiashara wa Kihindi na kuitumia bandari ya Zanzibar kama kitovu kikuu cha biashara. Uzalishaji wa karafuu na viungo uliimarika Unguja na Pemba na kuwa mazao makuu ya biashara. Kitovu cha Zanzibar kiliwavutia Wakoloni wa Kireno, Kiomani, Kijerumani na Kiingereza (Flint, 1965 & Sheriff, 1987). Hivyo, jamii ya Visiwa vya Zanzibar ina historia ndefu ya maingiliano ya kimbari baina ya Waafrika walio wengi na wanajamii kama vile wa Kihindi, Kiarabu na Kishirazi.

Waandishi wa fasihi wa Kiafrika hawakukwepa kusimulia mahusiano ya jamii zao ambazo mazingira na nafasi za kijamii zilibadilika kufuatia kupatikana kwa uhuru katika miaka ya 1960, katika nchi za ukanda wa Afrika ya Mashariki. Kwa jumla, matabaka ya kimbari yalishadadiwa na utawala wa Kikoloni wa Kiingereza na Usultani ambapo waliimarisha mgawanyo wa matabaka ya Waarabu kama wamiliki wa ardhi, walifuata Wahindi walikuwa wafanyabiashara na tabaka la chini lilikuwa la Waafrika waliokuwa wakitumikishwa (Flint, 1965: 651 & Sheriff, 2001: 302).

Wa Thiong'o katika riwaya yake ya *Petals of Blood* (1977), mbali ya kuzungumzia masuala mbalimbali ya Ukoloni na Ubaadakoloni katika jamii yake ya Kikuyu, amegusia pia suala la matabaka ya kimbari na migongano iliyojitokeza katika jamii yake hiyo. Kwa mujibu wa Cook na Okenimkpe (1987) wamemweleza mhusika Abdalla aliyepo katika riwaya tajwa ya Wa Thiong'o kuwa ni mtu aliyekuwa kiungo baina ya tajriba mahsusi wakati wa zamani (kabla ya uhuru) na wakati wa baada ya uhuru. Kuzaliwa akiwa chotara wa Kihindi ambaye kimaumbile hakukumfanya aache kubaguliwa baada ya uhuru, ingawa alikuwa mshiriki mkuu wa harakati za ukombozi wa Wakenya dhidi ya Wakoloni wa Kiingereza na vibaraka wao. Badala ya kupewa hadhi ya ushujaa, anabandikwa sifa ya "Raia wa makaratasi" au "Myahudi wa Afrika ya Mashariki". Wa Thiong'o anachukizwa na hali hiyo inayomkumba Abdulla na watu wa aina yake wanaokuja kuchukuliwa kuwa ni wageni wasiostahiki kuenziwa katika Kenya huru.

Si Wa Thiong'o peke yake analiyeliona tatizo hilo linalozikabili mbari za Kiasia na hata Kiarabu katika Afrika huru. Topan, katika tamthilia ya *Mfalme Juha* (1971), naye anayasawiri mazingira ya baada ya mabadiliko ya utawala ambapo wenyeji wameshika hatamu. Kupitia Walii na Salimu, anawataka wahame kuliko kuishi katika mazingira hatarishi na yasiyowatambua kihadhi watu wa aina yao. Hapa kunajitokeza sifa kubwa ya mgongano wa kimbari katika muktadha wa Ubaadaukoloni ambamo kuna msigano baina yao na sisi (Ashcroft, Griffiths & Tiffin, 2004).

Kupitia riwaya za Kizanzibari kama vile za *Asali Chungu* (Mohamed, 1989), *Dunia Mti Mkavu* (Said, 1947) na *Nyota ya Rehema* (Mohamed, 1978), masuala ya

migogoro ya kimbari katika muktadha wa Ubaadaukoloni yanaibuliwa na kuchanganuliwa na Flavia Traore (2008). Mazingira ya baada ya mapinduzi ya mwaka 1964 yanaibua migogoro na migongano ya kimbari. Katika *Asali Chungu,* hali ya mahusiano kabla ya mapinduzi ya 1964 baina ya kabaila wa Kiarabu aitwaye Zuberi na mtoto wake wa nje aitwaye Dude ambayo hayakuwa ya kupendeza kutokana na dharau za kikabila. Kuibuka kwa mapinduzi kunamuokoa asipate adhabu kutoka tabaka la Kiarabu. Hali hiyo inajitokeza katika riwaya ya *Nyota ya Rehema* ambapo Sulubu anaponea chupuchupu kuadhibiwa na mmiliki wake wa Kiarabu baada ya tabaka la juu kupinduliwa.

Glassman katika kazi yake ya *War of Words, War of Stones: Racial Thought and Violence in Colonial Zanzibar* (2011), ambapo anatoa hoja kuwa suala la fikra za Kitaifa na Kimbari za karne ya ishirini katika jamii ya Wazanzibari limechota kutoka vyanzo vingi, vikiwemo vya kiulimwengu. Aidha, Biersteker (2012) katika kuihakiki kazi hiyo ya Glassman anadai kuwa uchanganuzi wa fasihi ya Kiswahili umetoa fursa chache sana katika kuchanganua masuala ya kimbari, ingawaje mada hiyo iko wazi na inajitokeza katika kazi mbalimbali za kifasihi. Mawazo yake yametoa msukumo wa kufanyika utafiti huu. Utafiti wetu unaunga mkono mawazo ya mhakiki huyo Biersteker (2012) na unaona kuwa ipo haja ya kushughulikia pengo hilo katika uhakiki wa fasihi za Kibaadaukoloni za Zanzibar.

Utafiti huu una bainisha umuhimu wa Zanzibar kama mlango wa Afrika ya Mashariki na Mashariki ya Kati, Asia na Ulaya. Mseto huu wa mataifa na mbari umeacha urithi wenye mgawanyiko wa jamii zenye tamaduni mbalimbali visiwani Zanzibar. Ipo haja ya kulichanganua eneo la Zanzibar kupitia masimulizi ya kifasihi

ili kusuluhisha suala la siasa za utambulisho ambalo limejitokeza kwa wingi mara baada ya mapinduzi ya mwaka 1964 (Sheriff, 2001). Mulokozi (2017) anabainisha misingi mikuu ya Ubaadaukoloni kuwa mojawapo ni kupigania na kutetea utambulisho wa Mwafrika na kupinga ubaguzi wa kitaifa na kijamii, pamoja na usawiri hasi na potofu wa Mwafrika.

Uteuzi wa riwaya ya *Vuta N'kuvute* (1999) ya Adam Shafi na *Mungu Hakopeshwi* (2017) ya Zainabu Bahroon ni sehemu ya jitihada za kuliweka bayana suala la migongano ya kimbari katika jamii chotara ya Kizanzibar. Uhakiki wa fani na dhima mbalimbali kwa riwaya ya *Vuta N'kuvute* umefanywa (Diegner, 2011; Adam, 2014 & Wamitila, 2002 na 2008). Hata hivyo, katika kazi hizo, hakuna uhakiki na utafiti uliogusia masuala ya migongano ya kimbari katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*. Vilevile, kwa kadri ya ufahamu wa mtafiti huyu, riwaya mpya ya *Mungu Hakopeshwi* ya Zainabu Bahroon bado haijafanyiwa utafiti na hususani katika eneo la umbari lililotafitiwa katika tasnifu hii.

Mtafiti hakukusudia kuzilinganisha riwaya teule, ila zimetajirishana katika kutoa ushahidi wa kuwepo kwa matabaka ya kimbari Zanzibar na athari zake katika muktadha wa Ubaadaukoloni. Ingawa riwaya ya Shafi Adam Shafi ya *Vuta N'kuvute* (1999) na ya Zainab Alwi Bahroon ya *Mungu Hakopeshwi* (2017) zimepishana karibu miongo miwili, zote ni riwaya za Ubaadaukoloni katika muktadha wa Zanzibar. Kuna mchanganyiko wa jamii za kimbari za Kihindi, Kiarabu, Kizungu na Kiafrika. Mtafiti ameona ipo haja ya kujikita zaidi katika kuchunguza migongano ya kimbari katika kuleta utangamano kama jitihada za ujenzi wa Zanzibar mpya.

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Utangamano wa kimbari una changamoto mbalimbali zenye misingi ya kihistoria. Jitihada za ujenzi wa taifa moja na mbari moja ni changamoto wanazozishughulikia si wanasiasa pekee, bali hata wasanii. Suala hili limesawiriwa na waandishi wa kazi bunilizi za Ubaadaukoloni wa Zanzibar (Topan, 1971; Mohamed, 1978; Mohammed, 1983 Shafi, 1999; Haji, 2005; Shayo, 2011; Adam, 2014; Said, 2015 & Ali, 2017). Pamoja na wahakiki hao kuchunguza kazi hizi Zanzibar, suala la utangamano na migongano ya kimbari, bado halijatafitiwa katika riwaya teule. Utafiti huu ameona ipo haja ya kujikita zaidi katika kuchunguza migogoro ya kimbari katika jamii ya Zanzibar. Kwa hiyo, utafiti huu umechunguza migongano ya kimbari katika muktadha wa Zanzibar ya Ubaadaukoloni kwa kurejelea riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*.

### 1.4 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza migongano ya kimbari katika muktadha wa Zanzibar ya Baadaukoloni kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*.

#### 1.4.1 Malengo Mahsusi

Utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusi yafuatayo:

(i) Kubainisha makundi ya kimbari yanayoonekana katika jamii ya Zanzibar ya Baadaukoloni kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi.*

(ii) Kuchanganua aina za migongano ya kimbari ya jamii ya Wazanzibari wa Baadaukoloni kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi.*

(iii) Kutathmini mikakati ya utangamano wa kimbari inayopendekezwa na waandishi wa riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi.*

### 1.4.2 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu una maswali matatu:

(i) Kuna makundi gani ya kimbari kwa Wazanzibar wa Ubaadaukoloni katika riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi?*

(ii) Kuna aina gani ya migongano ya kimbari inayojitokeza katika jamii ya Wazanzibar ya Ubaadaukoloni kupitia riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi?*

(iii) Kuna mikakati gani ya kuleta utangamano wa kimbari inayopendekezwa na waandishi katika riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi?*

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unaweza kuchangia maarifa zaidi kuhusu uhusiano wa utambulisho, utangamano na umbari katika ujenzi wa jamii za Ubaadaukoloni. Pia, kubainisha masuala mbalimbali ya utangamano wa jamii na dini katika nchi huru zilizopitia Ukoloni mkongwe na zilizo na mazingira ya uchotara.

Vilevile, utafiti huu umeongeza taaluma katika hazina ya masuala ya kihistoria na yanavyoibuliwa kupitia fasihi. Marejeleo yatokanayo na utafiti huu yataiweka historia ya Zanzibar katika ramani ya nchi za dunia zenye kukabiliana na masuala ya uchotora na migongano ya kiutambulisho na jinsi inavyopambana. Pia, utafiti huu unaweza kusaidia watafiti na wataaluma kupata marejeleo katika uga huu wa fasihi.

Mwisho, utafiti huu ni muhimu kwa vile riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi* zinaibua masuala ya mapenzi baina ya wanajamii wa mbari tofauti ambapo mapenzi hayo yanasababisha kuibua changamoto za kibaguzi na pia kuleta

tumaini la utangamano baina ya wanajamii wanaojihisi kuwa wao ni wageni dhidi ya wenyeji. Dhana ya ugeni, kwetu, kwao, sisi, au wao huitia doa dhana ya uzalendo na utaifa. Riwaya hizi mbili teule zinapigania kuwepo kwa usawa na kutoa suluhisho la changamoto za kimbari.

## 1.6 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu umechunguza migongano ya kimbari katika muktadha wa Zanzibar ya Baadaukoloni kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*. Masuala yote yanayohusu migongano ya kimbari katika jamii ya Zanzibar yamerejelewa katika mjadala na uhakiki wa data zilizowasilishwa katika utafiti huu. Migangano ya kimbari imechunguzwa kwa kina namna ulivyosawiriwa katika riwaya teule. Riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi* ziliteuliwa kwa kuwa zina taarifa za kutosha zilizohitajika ili kukamilisha malengo ya utafiti yaliyobainishwa. Mjadala na uhakiki wa data zilizowasilishwa umeongozwa na nadharia ya Ubaadakoloni.

## 1.7 Mpangilio wa Tasinifu

Tasinifu hii inajumla ya sura tano zenye mada kuu na mada ndogo ndogo ndani yake. Sura ya kwanza inaelezea vipengele mbalimbali vya kiutangulizi. Vipengele hivyo ni usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahsusi ya utafiti na maswali ya utafiti. Vipengele vingine ni umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, na mpangilio wa tasinifu. Sura ya pili inaelezea mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu inahusu mbinu za utafiti. Sura ya nne, ya tano na ya sita inahusu uwasilishaji, mjadala na uchambuzi wa data za utafiti. Sura ya saba inahusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Katika sehemu hii, tumetalii kazi tangulizi zinazohusiana na mada ya utafiti huu ili kupata maarifa ya watafiti waliotangulia. Kazi tangulizi zimehusisha machapisho ya kila aina hasa vitabu, tasinifu na majarida. Lengo la kupitia kazi tangulizi ni kupata mwelekeo wa maarifa yanayohusiana na uchunguzi huu. Kwa mtazamo huo, sura hii ya pili inafanya mapitio ya maandiko na kufafanua kiunzi cha nadharia kitakacho ongoza utafiti huu unaohusu migongano ya kimbari katika muktadha wa Zanzibar ya Ubaadaukoloni kwa kuchanganua riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*.

## 2.2 Muhtasari wa Riwaya ya Vuta N'kuvute

*Vuta N'kuvute* ni riwaya iliyosawiriwa katika kipindi cha mwisho cha Ukoloni wa Kiingereza na Kisultani huko Zanzibar. Harakati za kutaka kujitawala zinajitokeza katika ngazi mbalimbali ikiwemo ngazi binafsi, ngazi ya kisiasa na kijamii. Msomaji anaelezwa maisha ya msichana wa Kihindi aitwaye Yasmin ambaye, kufutana na mila ya mbari yake ya Kiithnashiria, anaozwa kwa nguvu mume mzee na mfanyabiashara aitwaye Bwana Raza. Yasmin anajikuta akiishi maisha ya upweke na kutokuwa na furaha kiasi cha kulazimika kutoroka katika makazi yao huko Mombasa na kurudi Unguja.

Yasmin anaporudi Unguja, anafukuzwa na mjomba wake na kuamua kuishi na rafiki yake Mwafrika aitwaye Mwajuma. Yasmin anatengwa na familia yake akiwemo mama yake kwa kitendo cha kumtoroka mume wake na pia kuamua kuishi na

kutangamana na Waafrika na hivyo kuvunja mwiko mkubwa wa kutokuchanganyika baina ya mbari ya Kihindi na Kiafrika.

Tofauti za waziwazi baina ya jamii za Kihindi na Kiafrika zimesimikwa na wakoloni ambao walitumia mbinu ya kuweka matabaka na ubaguzi wa rangi katika jamii. Yasmin anaendelea kuvunja mwiko wa mbari yake anapokuwa na mahusiano ya kimapenzi na Mwafrika aitwaye Denge ambaye ni mwanaharakati wa kupigania ukombozi wa Waafrika. Wanafikia hatua ya kupata mtoto chotara katika mahusiano yao.

Yasmin anaandamwa na serikali ya Bwana Sayyid chini ya himaya ya Muingereza kupitia Inspekta Wright na Koplo Matata ambao wanamlazimisha Yasmin kumchunguza Denge na kuripoti nyendo zake. Yasmin anakataa kumsaliti Denge anayekuja kukamatwa na hatimaye kutoroka gerezani kwa msaada wa Bukheti, Yasmin na wanaharakati wenzake. Yasmin anakuja kuolewa na Bukheti kwa ridhaa ya familia yake na haswa mjomba wake aitwaye Gulam, ambaye naye amenasa kwa siri katika mtego wa kimapenzi na Mwafrika na kuzaa naye watoto. Hivyo, kuvunja mwiko wa kutangamana kimbari. Riwaya inamalizika kwa furaha ya harusi baina ya Yasmin na Bukheti huku akiimba nyimbo za Kihindi na taarab, akijikumbusha furaha ya kuwa huru.

Mwandishi anajenga hoja kuwa jamii yenye maingiliano kama ya Zanzibar, ambapo historia imesababisha kuwepo kwa Wahindi, Waarabu na Waafrika katika eneo moja haiwezi kukosa matabaka, hata hivyo utangamano hauwezi kukwepeka kwani wote

ni viumbe wanaoishi pamoja. Anapinga hali ya ubaguzi wa matabaka na mbari akisema:

> "Iko wapi heshima ya binadamu, ikiwa Muhindi anamwita Mswahili golo na Mswahili naye anamwita Muhindi ponjoro?" (Shafi,1999: 254).

Hitimisho hilo ndilo kiini cha utafiti wetu unaohusu migongano ya kimbari katika jamii ya Zanzibar ya ukoloni na Ubaadaukoloni.

## 2.3 Muhtasari wa Riwaya ya Mungu Hakopeshwi

Riwaya ya *Mungu Hakopeshwi* (2017) ni ya kwanza kwa mwandishi Zainab Alwi Bahroon, mzaliwa wa Mji Mkongwe Zanzibar. Riwaya hii ilitunukiwa tuzo ya Kiswahili ya Mabati-Cornell ya Fasihi ya Afrika mwaka 2018. Katika riwaya ya *Mungu Hakopeshwi*, Bahroon anachunguza na kukiangazia kipindi cha ubaadaukoloni, hususan mara baada ya mapinduzi ya mwaka 1964 huko Zanzibar. Katika riwaya hii, masuala ya kiuchumi, kisiasa, kitamaduni na kijamii yamemulikwa. Kuna migongano ya kisaikolojia yanayowakabili wahusika wakuu. Bw. Ahmed na mkewe Bi. Khadija ambaye ni Mwarabu, na watoto wake wanne ambao ni Said, Salah, Layla na Zahra. Bw. Ahmed pia alikuwa na mtoto mwingine chotara aliyeitwa Ahmed aliyezaliwa na Bi. Tunu ambaye ni Mwafrika.

Wahusika hawa wanasawiriwa wakikabiliana na migongano ya kimbari na kitabaka. Bw. Ahmed anajikuta akiwa hana utambulisho maalumu iwapo ni mgeni mhamiaji au mwenyeji na Mzanzibar. Athari za ukoloni katika mfumo wa uchumi na kiutamaduni, mfumo uliowapa fursa Waarabu na Wahindi dhidi ya Waafrika zinajitokeza hata mara baada ya Waafrika kujitwalia madaraka mara baada ya mapinduzi ya mwaka 1964.

Riwaya inaanza na mazungumzo baina ya Bw. Ahmed na mkewe Bi. Khadija ya kupokea posa ya binti yake Layla. Posa inatoka kwa ukoo wenye nasaba bora ya Kiarabu wa Bw. Haroub. Haroub anamposea mwanawe aliye mlevi na muasherati aitwaye Hafidh. Ndoa hiyo ni ya kuamuliwa na mzazi haimpi nafasi binti kuwa na maamuzi. Bw. Ahmed anaonekana akiwa mwenye mawazo na mwenye kulalamikia mahusiano ya kijamii kati ya wao Waarabu walio wachache na kundi la Waafrika, ambao ni watawala kwa sasa anaonesha utengano uliopo baina yao. Aidha, ndoa ya Layla na Hafidh inafanyika kwa nguvu huku ikigubikwa na misukosuko na mateso makubwa anayoyapata Layla ambaye anashindwa kutoroka au kuikwepa hadi mauti yanapomfika.

Said, mtoto mwingine wa Bw. Ahmed, anajiingiza katika mahusiano ya kimapenzi na msichana Farhat, ambaye ni chotara wa Kiarabu na Kisomali. Anapokataliwa na baba yake, Bw. Ahmed kumwoa msichana chotara, Said anaamua kuondoka nyumbani na kutoroka na Farhat hadi Dar es Salaam kuanza maisha yao ya kuishi wawili. Hata hivyo, baadaye Farhat anamkimbia Said kwa ukosefu wa fedha.

Siri ya maisha ya Bw. Ahmed kabla ya kuhamia Unguja inakuja kufichuka mara baada ya kijana chotara wa Kiarabu na Kiswahili, atiwaye Ahmed, kuja kumwomba kazi Bw. Ahmed na kukubaliwa na kuanza kuishi naye. Bi. Khadija anapendezwa na mwenendo wa Ahmed kiasi cha kutaka awe mkwe wake kwa kumwoza Zahra. Siri inafichuka kuwa Bi. Lulu, ambaye ni Mswahili wa Tanga, alimzaa Ahmed na Bw. Ahmed kabla ya kutorokea Unguja na kuja kuwa mfanyabiashara mkubwa. Hivyo, Bw. Ahmed anapogundua kuwa ameshindwa kuzuia hali ya mabadiliko na uchotara

katika familia na jamii kwa ujumla, anapatwa na mshtuko wa moyo na aibu kubwa kisha anafariki kwa kihoro.

Kupitia mazishi ya Bw. Ahmed Said na Hafidh wanaitumia fursa hiyo kupatana na kuungama makosa yao. Jitihada za Bw. Ahmed kujitenga na kuendesha maisha yake ya kutukuza unasaba wa Kiarabu zinasababisha kifo cha binti yake Layla aliyeolewa na Muarabu mwenye tabia mbaya na ukatili wa kupindukia. Kutokana na hulka ya Bw. Ahmed kutukuza unasaba kunamfanya mtoto wake wa kiume, Said, kumpinga na kuamua kutoroka nyumbani kwao na kumuoa Farhat aliye chotara wa Kiarabu na Kisomali. Utukuzaji wa nasaba ya Uarabu unamfanya Bw. Ahmed amkatae Ahmed aliye mtoto wake mwenye uchotara au ushombe wa Kiarabu na Kiafrika. Bw. Ahmed yeye mwenyewe anashindwa kuikwepa dhambi ya kuchanganya mbari kwani alishanasa katika mtego huo kwa Bi. Lulu. Anabainishiwa ukweli huo na mkewe Bi. Khadija kuwa sasa utambue kuwa ukoo wako ni mashombe (Bahroon, 2017: 216). Kiini cha migongano ya kimbari ndicho kiini cha utafiti tulioushughulikia kupitia kazi teule.

## 2.4 Zanzibar ya Wakati wa Ukoloni na Ubaadaukoloni

Mwaka 1821, Seyyid Said aliwakodisha Wabaluchi (Mabulushi), Washihiri, Wahindi, Waturuki na Washirazi kuja kuviteka visiwa na sehemu za pwani za Afrika ya Mashariki. Walipofanikiwa, walihamishia pia familia zao katika miji ya pwani katika sehemu ya Mombasa (Ngome ya Yesu), Saatenii katika mji wa Unguja na kisiwa cha Pemba. Aliwapeleka mamluki wengine wapatao 1500 katika mji ya Tabora na Kigoma kwenda kupigana na Chifu Mirambo wa Unyanyembe mnamo mwaka 1873 na kuanzisha himaya ya Sultani hadi Kongo Mashariki. Kutokana na

umuhimu wa Zanzibar kama kitovu cha biashara, Sultani Seyyid Said aliyekuwa mtawala wa Oman na Zanzibar aliamua kuhamishia makao yake makuu Zanzibar kuimarisha biashara yake katika mwaka 1840 (Chachage, 1996 & Sheriff, 1987).

Utawala wa Seyyid Said ulidumu hadi mwaka 1856. Kipindi hicho cha Sultani Said kilifanikiwa kujenga himaya kubwa yenye nguvu ambapo aliwakaribisha Wahindi na Waarabu kushiriki katika kilimo cha karafuu na minazi. Sultani Seyyid Said alipitisha sheria ya kumilikisha ardhi yenye rutuba kwa wafuasi wake wa Kiomani na Washirazi kwa ajili ya kilimo cha mikarafuu na minazi. Wahindi, pia walimsadia katika kuendesha kilimo cha kibiashara haswa katika kutoza ushuru wa forodha na kutoa mitaji ya biashara ya watumwa na pembe za ndovu kwa waliokuwa wanakwenda bara. Matokeo yake, biashara ya utumwa na pembe za ndovu iliimarika na kilimo cha karafuu na minazi kiliistawisha Zanzibar na masoko ya nje ikiwemo India na Ulaya (Adam, 2015; Oded, 2017 & Sheriff, 1987).

Bandari ya Zanzibar ilitembelewa na meli za Kidachi, Kiingereza na Kifaransa. Mshauri maalumu wa Sultani katika masuala ya biashara alitoka katika kampuni ya *The British East India Company.* Sultani Seyyid Said aliingia mkataba na Waingereza mnamo mwaka 1822 uliomtaka akomeshe biashara ya watumwa. Sultani Barghash ndiye aliyeweka sahihi mkataba huo mnamo mwaka 1873 kukomesha biashara ya utumwa. Masoko yote ya watumwa yalifungwa. Wamiliki wa watumwa walilipwa fidia na kuruhusiwa kuwapa uhuru watumwa. Sultani Seyyid Said alipata umaarufu mkubwa na kutambulika na mataifa ya Ulaya kama Uingereza kama Sultani wa Oman na Afrika ya Mashariki. Seyyid Said alikufa mwaka 1856, akiwaacha watoto wake wenye asili ya Kiomani, kwa upande wa baba na asili ya

Kihindi, Kishirazi, Kiarabu, Kiafrika na Kizungu, kwa upande wa mama, kama warithi halali wa kiti cha usultani (Pearce, 1920 & Romero, 2012).

Kiti cha usultani kilienda kwa watoto wake wakubwa, Majid (mama yake Muethiopia) kwa upande wa Zanzibar na Thuwain (Aliyezaliwa na mama mwenye asili ya Georgia) alitawazwa kuwa mtawala wa Omani. Kitendo hicho cha kugawanya usultani kilisababisha utengano kati ya himaya ya Omani na Zanzibar. Mwaka 1856, himaya ya sultani wa Zanzibar ilitenganishwa na kuwa na himaya za Omani na Zanzibar, Kilwa na Pemba. Waarabu wali imirisha biashara ya bara haswa ya utumwa na pembe za ndovu. Mtoto wa Seyyid Said, aiwatye Sultani Majid, alitawala hadi mwaka 1870 na kurithiwa na kaka yake, Barghash (mwana wa mama Muethiopia), aliyetawala hadi mwaka 1888. Sultani Seyyid Barghash aliwahi kuishi Bombay nchini India kwa muda wa miaka mitano uhamishoni. Katika kipindi hicho, aliathiriwa na utamaduni na desturi za vyakula, sanaa, muziki na usanifu majengo na pia alioa mwanamke wa Kihindi. Katika kipindi chake alifanikiwa kuiunganisha Pemba, Unguja na Tumbatu chini ya utawala wa moja kwa moja mara baada ya kifo cha Mwinyi Mkuu wa Dunga katikati ya Zanzibar na kifo cha Malkia wa Tumbatu Bi. Mwana Khadija. Katika kipindi cha utawala wa Barghash, Zanzibar ilikuwa na mahusiano ya karibu na Uingereza na India. Hadi kufikia mwaka 1886, kulikuwa na Wahindi wapatao 6000 katika Afrika ya Mashariki (Ingrams, 1967 Lodhi, 1973; Maurizi, 1984).

Mwaka 1873, jeshi la Uingereza lilimlazimisha Sultani Barghash kukubali kusitishwa kwa biashara ya utumwa mwaka 1885. Vilevile, Sultani Barghash alilazimishwa na Wajerumani kuachia madaraka ya utawala wake wa sehemu za bara

(Tanganyika) katika mkataba baina ya Waingereza na Wajerumani (*Delimition Treaty*), uliofanyika mwaka 1896, na ambao haukumhusisha Sultani Barghash. Mkataba wa *Heligoland-Zanzibar Treaty* wa mwaka 1890 uliifanya Zanzibar kuwa sehemu ya koloni la Waingereza. Upana wa himaya ya Zanzibar ulipunguzwa na kufikia kiasi cha upana wa maili kumi za ukanda wa pwani kutokea Mto Tana hadi Mto Ruvuma pamoja na visiwa vya Unguja, Pemba, Mafia, na Lamu.

Upande wa juu wa ukanda huo, nchi ya Uingereza na Ujerumani ziligawana milki na kuunda Koloni la Uingereza la Kenya na Tanganyika chini ya uangalizi wa Ujerumani. Wabelgiji walichukua sehemu ya Kongo Mashariki iliyokuwa ndani ya himaya ya Zanzibar, nao Wafaransa waliviweka visiwa vya Komoro chini ya utawala wao na hivyo kumnyang'anya Seyyid Barghash utawala wa visiwa hivyo. Baada ya utawala wa Sultani Barghash, kulifuatiwa na kaka zake wawili na hadi kufikia Sultani wa mwisho aitwaye Seyyid Jamshid aliyekuja kupinduliwa na Waafrika mwaka 1964 (Sheriff, 1987 & Vernet, 2009). Hivyo, Zanzibar ikawa ni ukanda wa makusanyiko ya mbari mbalimbali zilizodumishwa tofauti zake wakati wa ukoloni wa kisultani na wa Kiingereza kwa kuwa na matabaka ya Waarabu, Wahindi na Waafrika (Gray, 1975).

Mwaka 1963, serikali ya kikoloni ya Kiingereza iliendesha uchaguzi mkuu wa kwanza wa vyama vingi na ushindi ulienda kwa vyama vya ZPPP na ZNP vilivyokuwa na mrengo wa kisultani. Haukupita muda, serikali hiyo ilipinduliwa na Waafrika walio wengi chini ya chama cha ASP mnamo mwaka 1964 (Lofchie, 1965; Sheriff, 2001).

Katika muktadha wa ubaadakoloni katika ukanda wa Afrika ya Mashariki, tunaona sera za uzawa zikiimarishwa katika nchi ya Kenya, Uganda, Tanzania Bara na Visiwani (Zanzibar). Jamii ya Zanzibar imejipambanua kama jamii yenye uchotara, Uarabu, Uhindi na Uafrika. Makundi machache ya kimbari yenye asili ya Kihindi na Kiarabu bado yapo kama sehemu ya taifa jipya la Zanzibar baada ya mapinduzi ya mwaka 1964 yaliyowaweka Waafrika katika medani za utawala na kuwashusha wenye asili ya Kiarabu na Kihindi kuwa chini ya mamlaka ya umma wa waliowengi. Baada ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964, kulikuwa na jitihada za kuleta utangamano. Hata hivyo, Zanzibar ilikuwa bado imegawanyika katika makundi makubwa ya mbari za Waafrika, Wahindi, Waarabu na Machotara. Utambulisho wa wazi wa mbari za wahamiaji na wazawa ulikuwa upo katika maumbile ya kibaiolojia na kitamaduni. Jitihada za utangamao wa kimbari zilifanywa na serikali za baada ya ukoloni kwa kiasi kikubwa ingawa bado nyufa zilijitokeza.

Waarabu, Wahindi na waliokuwa wafuasi wa ZNP/ZPPP walilalamika kuhusu kutengwa kisiasa na kijamii kuanzia mwaka 1964 na 1972 na wengi wao walichukua ukimbizi (Chachage, 1996). Hali hii imezua migongano ya kiutambulisho katika kipindi cha ubaadaulokoloni.  Sehemu kubwa ya tabaka la Waarabu na Wahindi, ingawa walikuwa wachache kutokana na sera za kikoloni walikuwa ndio wenye kumiliki sehemu kubwa ya rasilimali kama vile ardhi na kuendesha biashara mbalimbali. Sehemu kubwa ya wafanyakazi wa mashamba hayo walikuwa Waafrika, hususani watumwa. Baada ya mapinduzi ya mwaka 1964, hali haikubadilika na ukandamizwaji uliripotiwa kufanyika kwa kipindi hicho (Chachage, 1996).

Hivyo, dhana ya umbari imejiimarisha katika muktadha wa Zanzibar huru, ambapo athari zake zinaibuliwa na wanafasihi wa Kiswahili. Katika kazi teule za kifasihi, makundi ya kimbari ya Kihindi (Kikoja, Kibaniani), Kiarabu (Washihiri, Waomani na Washirazi) na Wafrika na machotara yanabainishwa waziwazi kidesturi, kimila, kiitikidi na kimtazamo. Aidha, utangamano baina yao umeonekana kuwa ni suala tata lenye haja ya kusawiriwa kwa kina na wahakiki. Katika sehemu hii, tumepitia kazi tangulizi zinazodhihirisha namna jamii ya Wazanzibari wa wakati wa ukoloni na baada ya ukoloni walivyojumuika kama jamii ya mikusanyiko ya kimbari. Utawala wa Kisultani na ule wa Kiingereza ulipalilia kuwepo kwa mbari na utengano baina ya mbari za Kihindi, Kiarabu, Kizungu na Kiafrika. Pia kulizuka kizazi cha Machotara. Taarifa hizi za kihistoria zimeangaliwa katika uhakiki na uchambuzi wa riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*.

## 2.5 Masuala ya Kimbari kwa ujumla

Mada za kiubaadaukoloni katika fasihi ya Kiswahili na za Kiafrika si ngeni. Fasihi mbalimbali zimejihusisha na masula ya uhamiaji, utumwa, ukandamizaji, ukombozi, uwakilishi, ubaguzi wa rangi, utofauti na umbari Said (1978). Suala la ukombozi wa kiubaadaukoloni linahusu kunyakua maeneo ya kijiografia yaliyotawaliwa na pia kufufua utamaduni uliobeuliwa katika maandiko ya kwamba wazawa ni wavivu, wanyonge, na wanastahiki kutawaliwa. Fasihi za kibaadaukoloni zinaakisi masuala ya msigano wa kitamaduni, utafauti wa rangi na mbari mbalimbali. Fasihi hizo huathiriwa na michakato ya kibeberu kuanzia nyakati za ukoloni mkongwe hadi sasa na ni wajibu wa kazi hizo kupigania kuondolewa kwa usawiri hasi katika duru za elimu, jamii, sheria na siasa (Ashcroft na wenzake, 2004).

Kuna uhaba wa kazi za kihakiki za fasihi ya Kiswahili na Kiafrika katika kuchanganua masuala ya kiubaadaukoloni kupitia nadharia za Homi Bhabha (1990, 1994) zinazohusu masuala ya kichotara, hisia-kinzani (*ambivalence*) na uwanda-mpito (*liminality space*). Hata hivyo, zipo kazi chache zilizojikita katika suala la mgongano wa fasihi ya Kiswahili na Kiafrika. Ngugi wa Thiong'o aligusia suala la ubaguzi wa rangi na matabaka ya kimbari katika riwaya yake ya *Petals of Blood* (1977) ambapo mhusika Abdulla aliwakilisha mbari ya Kihindi. Katika tamthilia ya *Mfalme Juha* (1971), mwandishi Topan naye anamsawiri mhusika Salimu kama mhusika wa mbari tofauti aliyekuwa mfanyabiashara. Robert (1901-1962), aliyeishi wakati wa ukoloni wa Kijerumani na Kiingereza. Pia anatuonesha namna alivyokumbana na ubaguzi wa rangi katika mfumo ulioimarisha matabaka ya pembe tatu ya Wazungu kileleni, katikati Wahindi na mwishoni ni Waafrika katika tawasifu ya *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1991).

Mazingira ya matabaka ya kimbari wakati wa ukoloni yaliyoendelea wakati wa Ubaadaukuoloni yanaelezwa vizuri na Ricard (2000) katika kitabu cha *Swahili Theatre and Individualism* pale anapomzungumzia Ebrahim Hussein na kazi zake akiwa katika mitaa ya Dar es Salaam, ambapo jamii yake imegawanyika katika maeneo ya mbari ya Kihindi, Kizungu na Kiswahili. Anatuchorea jamii ya Kihindi katika mji wa Dar es Salaam ukiwa na athari za Uhindi kimajengo, kama vile hospitali, maduka, na hata shule. Mtazamo huu wa sura ya kijiografia unaoakisi tofauti za kimbari kimaeneo (Uswahilini, Uhindini, Uzunguni) unatusaidia pia katika uchanganuzi wa riwaya zetu teule za utafiti huu.

Maudhui ya migongano ya kitamaduni kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* (1999) yamegusiwa na Adam (2014) katika tasinifu yake ya uzamivu inayochunguza dhamira za kijamii na kiutamaduni katika riwaya za Kiswahili, inayotumia mifano kutoka riwaya ya *Kuli* na *Vuta N'kuvute.* Utafiti wetu unaunga mkono suala la kuwepo kwa matabaka ambayo yanabainishwa vyema kwa kutumia nadharia ya Ubaadakolonia ya Bhabha (1994).

Adam (2014) amejadili kwa kirefu kuwepo kwa matabaka, hususani ya Wahindi na Waswahili, kupitia tapo la Kimaksi. Anabainisha kuwa katika jamii ya Zanzibar, tabaka la Wahindi hujiona kuwa bora kuliko jamii ya Kiswahili. Hali ya matabaka inajidhihirisha katika hisia za wahusika ambapo Mwajuma alijenga dhana ya kuwa Yasimini ni "mtoto wa Kihindi, asingelipenda kuonekana amefuatana na mtoto wa Kiswahili kwa hofu kuwa Wahindi wenzake wasije wakamsema" (Shafi:1999: 33). Hali hii inaonyesha nyufa katika jamii ya Kizanzibar.

Ukweli kwamba matabaka yanashadidiwa na uhusuiano wa umiliki rasilimali lakini kwa jumla matabaka yote hayo ni zao la ukoloni na Ubaadaukoloni. Hivyo, matokeo ya kubaguana chimbuko lake ni mfumo wa ukoloni na Ubaadaukoloni. Adam (2014) anatoa hoja mantiki ya kubaguana, lakini halitazami suala hilo kwa jicho la mfumo wa Kiubaadaukoloni ambapo kupitia Bhabha (1994), tunayo fursa ya kuyadadavua masuala hayo kwa kuzingatia nadharia za uchotara, uhisi-kinzani, na uwanda-mpito.

Nadharia hizo zinatupa chimbuko na suluhisho la jamii ambayo tayari imekwishajijenga. Suluhisho si kuwakufukuza Wahindi na wageni wingine au kuliengua tabaka onevu na kubadilisha utawala, bali ni kwenda mbali zaidi na

kuangalia namna athari za ukoloni na ubaadaukoloni zinavyoweza kutatuliwa katika muktadha wa uchotara wa kijamii. Migongano ya kitabaka baina ya Yasmin na Mwajuma inatokana na saikolojia ambayo, tayari wawili hawa kila mtu anayo kutokana na makuzi na malezi aliyoyapata kutoka kwa wazazi na jamii yake kwa ujumla Shafi (1999). Suala hilo limetazamwa upya kupitia uwili au ukinzani badala ya kuangalia matokeo ya mfumo uliojengeka na namna ya kuzitatua changamoto za jamii mpya. Pengo hilo la kinadharia ndilo lililosukuma utafiti wetu uangazie tena riwaya ya *Vuta N'kuvute* pamoja na *Mungu Hakopeshwi* kwa jicho la nadharia za Ubaadakolonia.

Suala la ubaguzi wa rangi ambalo linahusiana moja kwa moja na migogoro ya kimbari limeelezwa na Musyoki (2016) kupitia utafiti wake unaoelezea maudhui ya ubaguzi katika kazi ya fasihi inayojulikana kwa jina la mhanga nafsi yangu. Kupitia utafiti huo imeelezwa kwamba, Ubaguzi wa rangi hasa kwa jinsia ya kike ndio swala tawala katika Mhanga nafsi yangu. Wanawake weusi ndio wanaoathirika zaidi na ubaguzi huu. Katika riwaya hii, aina hizi mbili za ubaguzi; ubaguzi wa rangi na ubaguzi wa kijinsia zinaingiliana, kwamba anayebaguliwa ni mwanamke mweusi. Hii inadhihirisha kwamba watu weupe ndio chanzo ubaguzi unaoendelea dhidi ya watu weusi.  Sigelman Lee na Susan Welch (1994) katika kitabu chao *Black Americans View of Racial Inequality*, wanathibitisha hili kwa kusema, maoni ya Wamarekani weusi kuhusu chanzo cha ubaguzi wa rangi kutokana na wenzao weupe.

Aidha, migogoro ya kimbari inasababisha ubaguzi ambao athari yake ni kuvunja mahusiano mema miongoni mwa wanajamii. Jambo hili limeendelea kuelezwa na Musyoki (2017), katika utafiti wake ameeleza kuwa ubaguzi husababisha kuharibika kwa uhusiano mwema ambao ungekuwa na manufaa kwa wahusika. Kama tujuavyo,

umoja ni nguvu katika kila sekta ya maendeleo. Kwa kutoa ufafanuzi alimrejelea muhisika Afida ambapo wanafunzi walipombagua darasani, hawakujua kuwa angeibuka mwanafunzi bora zaidi shuleni. Wangeungana na kushirikiana naye, angewasaidia kuimarisha masomo yao lakini walipombagua, hawakufaidi chochote kutoka kwa mwanafunzi bora zaidi shuleni.

Kazi hii imetufaa sana katika utafiti wetu kwani ni dhahiri kuwa ubaguzi anaozungumzia pakubwa Said A. Mohamed katika Mhanga Nafsi Yangu ni wa kirangi ambao unatokana na kuwepo mbari tofauti katika jamii ambazo ni zao la ukoloni. Tafiti hii imeshadidia hoja ya utafiti wetu huu inayoaminika kwamba suala la ubaguzi ambalo linatokana na athari za kikoloni bado linaendeleea na athari zake ni nyingi katika jamii nyingi zilizopitia kwenye mikono ya Wakoloni hata katika kipindi hiki cha baada ya ukoloni.

Thuranira (2017) katika utafiti wake unaohusu maudhui ya ukoloni mambo leo katika tamthilia teule za Kiswahili, ametumia nadharia ya ubaadaukoloni kupitia mhimili wake wa uibuikaji wa utamaduni mseto kwa mataifa yaliyotawaliwa. Katika utafiti wake amefafanua maudhui ya ukoloni mambo leo kwa kina, maudhui hayo yanaweza kutumiwa kama vichocheo vya kuwazindua viongozi wa Afrika kuanza kuzikabili athari hasi za ukoloni. Amemnukuu Said (1977) kwa kusema mataifa ya Kimagharaibi yalichukulia kuwa utamaduni wao ulikuwa bora kuliko wa mataifa ya Kimashariki na yale ya Kiafrika.

Utafiti huo umemsaidia mtafiti katika kulinganisha maudhui hayo na yale yaliyojitokeza katika riwaya ambazo ndio chanzo cha data za utafiti huu. Utafiti huo

uliofanywa, umeakisi yale yaliyoelezwa katika riwaya ya Mungu Hakopeshwi na Vuta N'kuvute juu jamii ya Wahindi kujiona wao ni bora na kuendelea kudumisha tamaduni zao kuoana wao kwa wao, lengo kuepuka kuingiliana na jamii nyingine za kiswahili ambazo zimetofautiana tamaduni.

Katika sehemu hii, tumebaini kuwa masuala ya changamoto za kimbari pamoja ubaguzi wa rangi unaonasibishwa na mbari yamegusiwa kwa kiasi fulani katika kazi chache za fasihi ya Kiswahili. Mgawanyo wa maeneo ya Uhindini, Uswahilini na Uzunguni unathibitishwa katika kazi hizo za Kiswahili na pia katika fasihi ya Kiafrika. Tafiti zinaonyesha kuwa katika jamii zilizopitia mikono ya Wakoloni, zinakabiliana na changamoto za kibaguzi ambazo zinatokana na rangi zao au hata nasaba zao. Historia ya Zanzibar inaeleza kuwa mbari ya Kihindi ilijishughulisha zaidi na biashara, mbari ya Kiarabu na Kizungu zilikuwa katika utawala na biashara. Mbari ya Waafrika imejikuta ikiwa sehemu ya wakulima na watumishi na kuwa ndio sababu ya kudharauliwa na watu wa jamii nyingine. Hali hiyo pia tumeikuta katika riwaya teule za utafiti huu. Kwa vile mifumo ya ukoloni haikufanya jitihada ya kuondoa mipaka ya kimbari, jamii ya *Vuta N'kuvute* na ile ya *Mungu Hakopeshwi* ya baada ya Ukoloni inajikuta ikiwa katika ufa uliosimikwa kwa muda mrefu.

## 2.6 Kiunzi cha Nadharia ya Ubaadakoloni

Fasihi za Kiubadaukoloni zinashughulikia masuala ya utambulisho wa wanajamii na masuala ya uzawa katika muktadha wa ukoloni na baada ya ukoloni. Wananadharia mbalimbali kamavile Frantz Fanon, Ngugi wa Thiong'o,V. S. Naipaul, na Homi Bhabha wamejishughulisha na nadharia za Ubaadaukoloni. Ubaadakoloni ni kiunzi cha nadharia kinachochambua, kuelezea, na kuangalia athari za ukoloni na ubepari

katika nchi zilizotawaliwa, hasa nchi za ulimwengu wa tatu. Inaangazia matatizo waliyopitia wanajamii kutokana na kutawaliwa na unyonyaji uliofanywa na wakoloni (watawala) pamoja na kuchukua ardhi ya wazawa. Utafiti huu umekitwa kwa mwananadharia Homi Bhabha (1994). Huyu ni mwanazuoni na mwanafalsafa ambaye mawazo yake yanalenga katika nadharia ya Ubaadakoloni.

Bhabha (1994) amekuwa kiungo muhimu katika kuzungumzia ubaadakoloni na alihamasishwa na wanaumuundoleo wa Kimagharibi na wananadharia, akiwemo Jacques Derrida, Jacques Lacan na Michel Foucault. Katika kitabu chake cha *Nation and Narration* (1990), amezungumzia mazoea ya kuzifanya nchi za ulimwengu wa tatu kuwa na tabia zinazofanana. Kwa kufuata lenzi ya Bhabha, suala la utambulisho na utamaduni wa watawaliwa haliwezi kutenganishwa na suala la utamaduni wa watawala. Katika kufafanua suala la ubaadakoloni, Bhabha ameibua dhana mbalimbali katika kitabu chake cha *The Location of Culture* (1994), kama vile wigo (*mimicry*), uchotara, uwanda wa tatu (*third space*), hisia-kinzani, ugeni (*unhomely*) uwanda-mpito na nyinginezo. Nia yake ni kuondosha fikra za uwili katika nyanja za utamaduni. Dhana alizopendekeza ni jitihada za utetezi wa makundi gandamizwa (*subaltern*) ambayo yapo nje ya nguvu za kisiasa, kijamii na kijiografia za koloni na nchi za kikoloni. Haya ni makundi yanayokosa sauti ambayo, kwa muundo wa ukoloni na Ubaadaukoloni, wamebambikwa sifa hasi na za unyonge na ukatili. Kundi hilo huakisiwa kama “wao” dhidi ya “sisi”. Msingi wa ukoloni ni uwili wa kibaguzi wa “wao” dhidi ya “sisi”.

Dhana hizi zote zinaelezea juhudi za watawaliwa katika kupinga nguvu (mamlaka) za wakoloni. Bhabha anaeleza kuwa tusiangazie ukoloni kama mfumo nyonyaji,

kandamizi, tawala pekee, bali kama mfumo wenye tabia ambatani na mwingiliano wa tamaduni mbalimbali. Maandiko yake yamesaidia pakubwa katika kujifunza fasihi na nadharia ya utamaduni kutokana na uhifadhi wa nyaraka mbalimbali zinazohusu ukoloni. Bhabha (1994) amezungumzia kuhusu historia ya ukoloni na hali ilivyo kwa sasa.

Mtafiti ameteua dhana kuu tatu za nadharia ambazo ni  uchotara, uhisia-kinzani na uwanda-mpito katika ukusanyaji wa data, uchambuzi wa data na kujaribu kujibu maswali ya utafiti. Muktadha wa Ubaadaukoloni wa Zanzibar kupitia riwaya teule, umechambuliwa kupitia kiunzi cha nadharia ya Ubaadakoloni ya Homi Bhabha. Bhabha anaamini kuwa utamaduni wa watawala (wakoloni) umewekwa kwa ajili ya kuwafanya watawaliwa kufuata utamaduni huo. Kipindi cha ukoloni na Ubaadaukoloni kimeathiri watawaliwa kwani suala la wigo limeonekana sana pale watu wa jamii fulani iliyotawaliwa, kwa mfano Afrika, kuiga lugha, mavazi, siasa (utawala) au masuala yote ya kiutamaduni kutoka kwa watu waliowatawala,kama vile Waingereza, ili wafanane nao. Ukoloni umetengeneza uchumi ambao watawala na watawaliwa wanategemeana. Watawala wamekuwa wakianzisha vitu mbalimbali wakitarajia watawaliwa wawajibike kuvitekeleza

Athari za Ukoloni katika nchi za Ubaadaukoloni kama ilivyo Zanzibar ni sehemu muhimu ya uchanganuzi wa riwaya teule za utafiti huu. Historia inaonyesha kuwa matukio yanayojitokeza katika riwaya teule yanauthibitisho katika historia nzima ya Zanzibar na mandhari inayosimuliwa katika kazi bunifu teule za Shafi na Bahroon. Hali hii inapelekea kuibainishia hadhira dhima mojawapo ya riwaya teule kuwa ni kielelezo cha historia ya Zanzibar na nchi za dunia ya tatu.

## 2.7 Namna Dhana za Homi Bhabha Zilivyotumika katika Utafiti Huu

Migongano ya kimbari kwa wahusika katika riwaya teule imejadiliwa kupitia dhana za Kiubaadaukoloni alizopendekeza (Bhabha, 1994). Kwa vile utafiti huu unahusu changamoto za kimbari katika jamii ya Wazanzibar kama ilivyosawiriwa katika riwaya teule, nadharia za Ubaadaukoloni za Bhabha (1994, 1996), kupitia dhana kuu tatu za uchotara, hisia-kinzani na uwanda-mpito, zimesadifu kutumika vizuri katika utafiti huu.

### 2.7.1 Uchotara

Dhana ya uchotara ni ujumuisho wa utamaduni au desturi. Hali ya kikundi cha watu kuwa na sifa za utamaduni zaidi ya mmoja. Kwa mujibu wa Bhabha (1994) uchotara ni mfumo mpya unaopinga muegemeo wa upande mmoja. Uchotara unaweza kutokea kwa namna mbalimbali. Kuna uchotara wa kilugha, uchotara wa kimbari na uchotara wa kidini. Katika muktadha wa Zanzibar, uchotara wa lugha moja kuingia katika lugha nyingine huhusu lafudhi na lugha za Kiarabu, Kihindi, au Kiingereza kupenya katika lugha ya jamii ya Kiubaadaukoloni. Hivyo, nadharia ya Bhabha ya uchotara inazaa utambulisho mpya na ukinzani wa kitamaduni, nayo inakidhi haja ya kinadharia katika kuchambua masuala mbalimbali ya migongano ya kimbari katika riwaya teule.

Tumeteua nadharia ya uchotara kwa vile, katika riwaya za Ubaadaukoloni za Zanzibar, wengi wa wahusika wake wana mseto wa utamaduni au desturi. Japo wakazi asilia ni makabila ya Waswahili (Wapemba, Watumbatu na Wahadimu), baadaye jamii au makabila hayo yalianza kuingiliana na jamii nyingine. Watu wanaotajwa kuingiliana na wakazi wa Magharibi mwa Bahari ya Hindi au Pwani ya

Afrika Mashariki ni Waarabu, Waajemi, Wahindi, Wachina, Washirazi, na Wazungu (Lodhi, 1973; Sheriff, 2001). Mwingiliano ulikuwa katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii.

Bhabha (1994) anaeleza kuwa kubadilika na kupokea utamaduni mwingine kunaweza kuwa na faida, kustawisha, na kumbadilisha mtu, lakini pia kunaweza kuchukuliwa kama ukandamizaji. Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*, tunachunguza kuwepo kwa mbari mbalimbali kunakosababisha kuwepo kwa mwingiliano wa kitamaduni katika jamii ya Zanzibar, athari zake na suluhisho lililosawiriwa katika kujenga utangamano.

### 2.7.2 Hisia-Kinzani

Bhabha (1994), katika kitabu chake cha *The Location of Culture*, anaangazia hisia-kinzani pale mtu anapojisikia kuwa na ukinzani wa kimaono au haiba. Ni rahisi mtu kupata vurugu za maono pale anapotaka kujizoesha na mazingira ya tamaduni mpya. Mazingira ya Ubaadaukoloni huibua kanuni na tabia mpya za kijamii kiasi cha kuwafanya wahusika kujisikia kuwa na hisia-kinzani. Jamii au kikundi kinaweza kujikuta kikiwa katika mazingira mapya ya kisiasa na kiuchumi kiasi cha kuvurugikiwa maono.

Hali hii ya kubaini uhisia-kinzani inatusaidia katika uchambuzi wa riwaya teule kwa vile mazingira ya Zanzibar yanaibua hisia-kinzani kwa wenyeji pale wanapolazimika kuchagua mila na itikadi zilizorithiwa kutoka enzi hizo kabla ya mapinduzi au kufuata uoni wao. Kwa mujibu wa Bhabha (keshatajwa), nchi za Ubaadaukoloni zinajikuta zipo katika hali ya uhisia-kinzani wa Kiubaadaukoloni.

Hata hivyo, tofauti na wahakiki Abussamen na Neimneh (2018) ambao walichunguza hisia-kinzani kupitia mwandishi wa kazi bunifu, mtafiti amejikita katika hisia-kinzani binafsi zinazowakuta wahusika katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*. Lugha ya wahusika na matendo yao hutumika katika riwaya teule kama vielelezo vya uhisia-kinzani unaowakumba wahusika wakuu. Katika kuibua maudhui, tumejishughulisha zaidi na kuchanganua matini, hususani namna wahusika walivyosawiriwa badala ya kumchanganua mwandishi. Msingi huu umesaidia kufafanua lengo mahususi la pili la utafiti la kuchanganua aina ya migongano ya kimbari kwa kubainisha hisia-kinzani zilizowakumba wahusika wa riwaya teule na kusababisha migogoro na mabadiliko katika jamii.

### 2.7.3 Uwanda-Mpito

Bhabha (1996) anabainisha kuwa uwanda-mpito ni kipindi cha mpito ambacho uchotara huzaliwa. Anasisitiza umuhimu wa nafasi ya uwanda-mpito ambapo mawazo mapya au uoni mpya huibuka na mabadiliko ya kitamaduni hujitokeza. Katika hakiki za kiubaadaukolonia, uwanda-mpito huwakilisha mipaka inayogawa nyanja mbili za kiutambulisho; mathalani, Mwarabu na Mswahili au lugha ya Kiarabu na Kiswahili.

Homi Bhabha, katika kitabu chake cha *Location of Culture* (1994), anaitaja dhana ya mpito kuwa inasifa za utata, uchotara, na mabadiliko. Hali ya mpito huwakumba watu au kikundi kilicho katika hatihati na wasiojielewa wako katika hatua ipi ya maendeleo. Ni watu au kikundi kinachojisikia kutengwa, bila utambulisho maalumu au nguvu ya ushawishi (Thomassen, 2006). Uhakiki wa Abussamen na Neimneh

2018) umebaini muktadha wa uwanda-mpito wakati wa kujadili uchotara na hisia-kinzani katika kazi hiyo.

Kazi mojawapo ya fasihi ya Kiafrika inayojadili kwa kina nadharia ya uwanda-mpito inapatikana katika riwaya za Botswana. Utafiti wa shahada ya uzamivu wa Kalua (2007), uitwao "*The Collapse of Certainty: Contextualizing Liminality in Botswana Fiction and Reportage*", unachangia maarifa juu ya matumizi ya nadharia hii katika uhakiki wa kifasihi. Katika utafiti huo, Kalua anaitumia nadharia ya Bhabha kuchambua kazi za waandishi mashuhuri wa riwaya wa Botswana waitwao Unity Dow na Alexander McCall Smith. Kalua ameonyesha namna Botswana ilivyobadilika kutoka mfumo dume wakijadi hadi kuwa na mfumo mpya wa utambulisho unaowapa wanawake sauti baada ya uhuru.

Matumizi ya nadharia ya uwanda-mpito ya Bhabha (1994) katika kazi mbalimbali ikiwemo uhakiki wa Kalua, unatupatia ushahidi wa kuitumia nadharia hiyo katika riwaya za Zanzibar, nchi ambayo haina tofauti na Botswana. Nchi zote mbili zimetawaliwa na wakoloni wa Kiingereza. Wananchi wake na waandishi pia wanapitia kipindi cha uwanda-mpito kilicho na mseto wa utamaduni na mkanganyiko wa utambulisho. Katika utafiti huu, tumejikita katika uchanganuzi wa hali hiyo ya uwanda-mpito pamoja na athari zake kwa wahusika wa riwaya teule.

## 2.8 Muhtasari

Sura hii imejikita katika kuchanganua mapitio ya kazi tangulizi za watunzi na kiunzi cha nadharia. Tumebaini kuwa mazingira ya matabaka ya kimbari yalianzia kipindi cha ukoloni na kuendelea mpaka kipindi cha Ubaadaukoloni. Vilevile, changamoto

za kimbari zimeelezwa kwa ufupi kulinganisha na ukubwa wa changamoto na unavyoibuliwa na waandishi wengi wa Zanzibar. Aidha, tumeteua nadharia ya Ubaadaukoloni ya Homi Bhabha katika maeneo ya uchotara, uhisia-kinzani na uwanda-mpito. Tumebaini namna baadhi ya kazi za fasihi za Kiafrika zilivyojihusisha na matumizi ya kiunzi hiki cha nadharia katika kuhakiki kazi za fasihi. Tumeona kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kutumia nadharia hii katika fasihi ya Kiswahili ili kuibua masula ya kimaudhui na hata yale ya kifani katika kuhakiki kazi hizo.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imeeleza mbinu za utafiti zilizotumika katika tasinifu hii. Hivyo, sura inafafanua eneo la utafiti, kundi lengwa, mbinu za kukusanya data na mbinu za uchambuzi wa data za utafiti. Mbinu hizo zilimwezesha mtafiti katika ukusanyaji na uchambuzi wa data zilizowasilishwa na kumwezesha kufikia malengo ya uchunguzi uliofanyika.

## 3.2 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti ni mahali ambapo mtafiti hukusudia kutafuta data kwa ajili ya kukamilisha malengo ya utafiti wake (Kothari, 2009). Aidha, eneo la utafiti huteuliwa kulingana na lengo kuu la utafiti. Utafiti huu ni wa maktabani. Kwa hiyo, taarifa za msingi za utafiti uliofanyika zimepatikana kwa kusoma riwaya teule ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*. Riwaya hizo zilituwezesha kupata data zilizokusudiwa katika utafiti huu.

## 3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mpango wa utafiti unaoonesha sura ya uchunguzi unavyotakiwa kufanywa kuanzia hatua ya ukusanyaji wa data mpaka hatua za uandishi wa ripoti ya utafiti (Baradyana & Ame, 2005). Mpango huo huonesha namna data zitakavyokusanywa katika utafiti unaohusika. Katika uchunguzi huu mbinu ya uchunguzi kifani imetumika. Mbinu hii humruhusu mtafiti kuchagua eneo mahsusi atakalolishughulikia katika utafiti wake. Kwa hiyo, uchunguzi kifani katika utafiti huu ni riwaya teule ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*. Uteuzi huo ulimpa

fursa mtafiti kukusanya data za kutosha ili kukamilisha utafiti wake. Jambo hili linatokana na kwamba mtafiti alikuwa na muda wa kutosha kulichunguza jambo lililoshughulikiwa.

### 3.4 Vyanzo vya Data za Utafiti

Utafiti ulikuwa ni wa kimaktaba. Kwa msingi huo, data za msingi katika utafiti huu zilikusanywa kwa kusoma kutoka katika riwaya zilizohakikiwa za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*. Kwa kawaida, data za msingi ni zile ambazo hazijawahi kukusanywa na mtu mwingine kwa wakati huo na kufanyiwa kazi katika utafiti mwingine (Kothari, 2004). Riwaya zilizorejelewa zilimwezesha mtafiti kukamilisha malengo ya utafiti uliofanyika.

### 3.5 Uteuzi wa Watafitiwa

Watafitiwa huelezwa kuwa ni washiriki wote, binafsi au kundi ambalo mtafiti hulitumia kwenye utafiti wake ili kupata data zilizolengwa. Watafitiwa ni sehemu ya watu au vitu vinavyotarajiwa kumwezesha mtafiti kupata data za utafiti wake ili aweze kutimiza malengo ya utafiti anaokusudia (Ponera, 2019). Katika utafiti huu, mtafiti ametumia mbinu ya uteuzi lengwa ili kupata riwaya mbili zilizomwezesha kupata data za msingi za utafiti uliofanyika. Riwaya teule zilizolengwa na kushughulikiwa katika tasinifu huu ni ile ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*. Mbinu ya uteuzi lengwa ilimsaidia mtafiti kupatikana kwa data za msingi za utafiti huu.

### 3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Data za tasinifu hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini na ile ya uchambuzi wa nyaraka.

### 3.6.1 Mbinu ya Usomaji Makini

Mbinu ya usomaji makini ni mbinu mojawapo inayomruhusu mtafiti kukusanya data za utafiti uliolengwa baada ya kusoma matini iliyokusudiwa. Mtafiti hupata data za msingi zinazohusiana na malengo mahsusi ya utafiti wake baada ya kusoma kwa kina matini teule (Creswell, 2009). Katika utafiti huu, mbinu ya usomaji makini ilitumika kukusanya data zilizolengwa kwa kuzingatia malengo mahsusi ya utafiti. Mtafiti alilazimika kuandaa shajara iliyokuwa na mada iliyohusiana na malengo mahsusi ya utafiti. Mtafiti alizisoma riwaya zilizoteuliwa za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi* kama zilivyokwishaelezwa, kisha kunukuu taarifa zinazohusiana na malengo ya utafiti na kufanya uchambuzi. Tazama kiambatanisho namba moja kwa maelezo zaidi.

## 3.7 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data ni kitendo cha kupanga data ili kusaidia kujibu maswali ya utafiti (Robson, 2007; Ponera, 2019). Uchambuzi wa data hufanywa kwa kuongozwa na mbinu zinazokubaliwa kwa ajili ya kazi inayoshughulikiwa. Baada ya kukamilika kwa zoezi la ukusanyaji wa data zilizolengwa, mtafiti hutakiwa kuzichambua na kuziwasilisha katika ripoti ya utafiti. Uchambuzi wa data katika utafiti huu uliongozwa na mbinu ya uchambuzi wa kimaelezo. Mbinu ya kimaelezo humpa nafasi mtafiti kuvielewa vipengele vinavyoshughulikiwa katika kazi iliyolengwa. Katika utafiti huu, mtafiti alipata nafasi ya kuzichunguza riwaya zilizoteuliwa za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi* kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Data zilikusanywa kulingana na malengo ya utafiti kisha kuziwasilisha kwa kuzitolea maelezo. Tazama kiambatanisho namba mbili kwa maelezo zaidi.

### 3.8 Usahihi na Ubora wa Data

Usahihi wa data ni utaratibu unaowezesha kupatikana kwa data za kuaminika na zilizo bora Morrison (2000). Usahihi wa data za utafiti unatokana na uwezo wa mbinu za utafiti kutoa matokeo yale yale pindi uchunguzi unaporudiwa kwa kutumia njia zile zile. Mtafiti alikusanya data kwa kutumia mbinu ya usomaji wa matini na ile ya uchambuzi wa nyaraka. Uchambuzi wa data uliongozwa na nadharia za Ubaadaukoloni. Mbinu za kimaelezo ilitumika katika uchambuzi wa data zilizowasilishwa. Kwa kufanya hivyo, udhaifu wa mbinu moja ulikamilishwa na ubora wa mbinu nyingine. Mjadala kuhusu usahihi na ubora wa mbinu zilizotumika ulifanyika kati ya mtafiti na msimamizi wake. Usahihi na ubora wa data katika utafiti huu ulihakikiwa kwa kutumia nadharia iliyoongoza mjadala wa data, mbinu za ukusanyaji na uchambuzi wa data zilizowasilishwa katika tasinifu hii.

### 3.9 Maadili ya Utafiti

Miongoni mwa vitu muhimu anavyotakiwa kuvizingatia mtafiti ni maadili ya utafiti. Maadili ya utafiti yanayohusu kupata kibali cha kufanya utafiti pamoja na kutunza siri za watafitiwa. Katika utafiti huu, maadili ya utafiti yalizingatiwa kabla na baada ya kukusanya data. Kwa kuwa utafiti wetu ulikuwa ni wa maktabani, tulihakikisha kuwa hisia binafsi zinaepukwa. Mtafiti aliegemea kwenye madondoo kutoka katika riwaya teule na kuchambuliwa kifasihi kwa kuongozwa na malengo mahsusi ya utafiti huu.

Katika utafiti wa kitaaluma, mtafiti hatakiwi kujikita upande wowote katika hatua zote za utafiti ili kutoa taarifa ya kuaminika katika kukamilisha utafiti wake. Kuegemea upande mmojawapo kuhusiana na matokeo ya utafiti ni kinyume na

maadili ya taaluma ya utafiti. Mtafiti anapaswa kutoa taarifa kwa usahihi yenye kuaminika kwa kufuata kanuni na taratibu za utafiti wa kisayansi. Katika utafiti huu wa kimaktaba, mtafiti aliandaa na kuandika taarifa ya utafiti kulingana na data za msingi zilizopatikana katika riwaya zilizolengwa kwa kurejelea baadhi ya machapisho yaliyowiana na malengo mahsusi ya utafiti.

## 3.10 Hitimisho

Mbinu za utafiti zimewasilishwa katika sura hii. Baadhi ya vipengele vilivyochunguzwa katika sura hii ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, vyanzo vya data, watafitiwa, mbinu za ukusanyaji wa data na mbinu za uchambuzi wa data. Mbinu hizo zilimsaidia mtafiti kupata data zilizolengwa kulingana na malengo ya utafiti. Mbinu hizo zilikamilishana katika hatua zote za ukusanyaji, uchambuzi na mjadala wa data uliofanyika katika sura ya nne, ya tano na ya sita. Sura ya nne inayofuata inahusu mjadala wa data zilizowasilishwa katika tasinifu hii.

# SURA YA NNE

# KUBAINISHA MAKUNDI YA KIMBARI KATIKA JAMII YA ZANZIBAR YA BAADAUKOLONI KUPITIA RIWAYA YA VUTA N'KUVUTE NA MUNGU HAKOPESHWI

## 4.1 Utangulizi

Utafiti huu ulichunguza migongano ya kimbari katika riwaya ya *Mungu Hakopeshwi* na *Vuta N'kuvute*. Sura hii ilikusudia kutimiza malengo mahsusi la kwanza. Lengo mahususi la kwanza lilihusu kubainisha makundi ya kimbari yanayoonekana katika jamii ya Zanzibar ya baadaukoloni kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*. Uchambuzi wa data na mjadala wa matokeo katika utafiti huu umeanza kwa kuelezea muhtasari wa riwaya teule.

## 4.2 Makundi ya Kimbari Yenye Migongano katika Jamii ya Wazanzibari

Lengo mahususi la kwanza la utafiti huu lilikuwa kubainisha makundi ya kimbari yaliyojitokeza katikamuktadha wa ubaadaukoloni katika taifa la Zanzibar kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi.* Kwa mujibu wa nadharia ya Ubaadaukolonia mfumo wa Ukoloni ulikuwa ni wa uwili, yaani "sisi" dhidi ya "wao". Mfumo huu umeacha athari kubwa kwani watawaliwa wameendelea na mfumo ule wa uwili na kusababisha makundi mbalimbali ambayo yanatokana na athari za kikoloni. Kila kundi limekuwa likijinasibu na kutambulika kwa vibainishi vyake. Mtafiti kwa kutumia vibainishi alivyobainisha mwandishi wa riwaya. Katika kubainisha makundi hayo, mwandishi amenukuu baadhi ya aya ambazo zinathibitisha hoja hii ya kusawiriwa makundi ya kimbari katika riwaya hizi teule.

Kupitia wahusika na uhusika wao wa riwaya hizi teule. Mtafiti amebaini kuwa kila kundi limekuwa likijiona bora dhidi ya jengine.

Uhusika wa wahusika ni mbinu inayotumiwa na mwandishi kuwasawiri na kuwashirikisha kimatendo wahusika katika kazi yake. Hali hii pia huweza kumsaidia mchambuzi au mhakiki wa kazi ya fasihi kuibua dhamira mbalimbali. Kyando (2013) anaeleza kuwa uteuzi wa majina ya wahusika katika kazi za riwaya hufanywa na mtunzi kwa namna ambayo jina la mhusika litafanana na kile ambacho anakifanya, tabia zake, maumbile yake, mahusiano yake na wenzake na kadhalika. Katika kufanya hivyo, mtunzi anapata mhusika au wahusika sadfa. Waandishi wamewasawiri wahusika kwa kutumia majina, lugha zao na maumbile yaliyosababisha kuibuka makundi  ya kimbari ya aina tofauti

### 4.2.1 Kundi la Waafrika au Waswahili

Katika riwaya hizi, waandishi wamewachora wahusika ambao wamewakilisha kundi la Waafrika. Mathalani, katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* (1999), kuna wahusika kama Mwajuma, Denge, na Koplo Matata. Majina haya ya wahusika ni majina yanayotumiwa katika jamii za Kiswahili na Kiafrika. Aidha, uhusika wao katika harakati za kuikomboa nchi yao kutoka kwa Wakoloni unadhihirisha Uafrika wao. Mathalan, Denge alikuwa anajali zaidi harakati zake za ukombozi kuliko mapenzi. Mwandishi anaeleza:

> "Alichukua moja na kumpa Mambo "soma" alimpa karatasi moja iliyokuwa imechapwa kwa maandishi makubwa. Alisoma, "kufa au kupona tunataka uhuru"  (Shafi , 1999: 166).

Koplo Matata alikuwa askari aliyekuwa akitumwa na Wakoloni kuwafwatilia Waafrika ambao walikuwa katika harakati za kutaka uhuru wa nchi yao. Wasifu wa askari unathibitisha kuwa yeye alikuwa Mwafrika. Mwandishi anaeleza:

> "Alisimama kwa mbali na alihakikisha kwamba Yasmin amemwona kwani tambo lake na weusi wa rangi yake vilitosha kumfanya aonekane waziwazi pale aliposimama" (Shafi, 1999: 136).

Vilevile, Mwajuma alikuwa anaishi na rafiki yake Yasmin. Mwajuma alikuwa Mswahili na akiishi Uswahilini. Mwandishi anaeleza kuhusu Yasmin alivyokuwa anaishi, anasema "Yasmin amezama katika maisha ya Uswahilini….Si kama aliyazoea maisha tu, bali na Waswahili wenyewe" (Shafi, 1999:37).

Kwa upande wa riwaya ya *Mungu Hakopeshwi* Bahroon (2017) naye amewachora wahusika kuwakilisha kundi hilo la Waafrika. Wahusika hao ni kama vile Bi. Tunu, Bi. Mwanawetu, pamoja na wafanyakazi wa Bw. Ahmed. Hili ni kundi la Waswahili ambalo limetofautiana na makundi mengine kiasili na kibaiolojia na kujinasibu kuwa wao ndio wenye nchi na raia halali. Uafrika wa wahusika hawa unadhihirika kwa wafanyakazi wa Bw. Ahmed walipokuwa wakimsema Ahmed na Bw. Ahmed. Anaeleza:

> "Siku zote sisi ni watumwa kwenye upeo wa macho yao na wao ndio watawala. Wametoroka kwao kwa ngalawa wakiwa wamevaa vishuka tu. Sasa wamekuwa jeuri katika nchi ya watu" (Bahroon , 2017: 146).

Vile vile, katika riwaya ya Mungu hakopeshwi, mhusika Sada anawakilisha kundi hili la Waswahili. Wakati anazungumza na Hafidh (Muarabu), Sada anamwambia Hafidh kuwa haamini kuwa kweli Hafidh anampenda kwa sababu yeye ni Mswahili na Hafidh ni Muarabu Bahroon (2017:175). Ukoloni uliacha athari ya kuendelea

kuwagawa wanajamii hata baada ya ukoloni. Waafrika waliendelea kutumwa na Waarabu na Wahindi kama ambavyo imeelezwa katika riwaya ya *Mungu Hakopeshwi.*

### 4.2.2 Kundi la Waarabu

Hili ni kundi lingine ambalo limeundwa kupitia wahusika mbalimbali katika riwaya hizi teule. Katika riwaya ya *Mungu Hakopeshwi* mwandishi amewachora wahusika kama familia ya Bw. Ahmed, ambao ni mke wake Bi. Khadija, pamoja na watoto wake wanne, ambao ni Said, Layla, Zahra na Salah. Vilevile, kuna familia ya Bw. Haroub pamoja na mtoto wao Hafidh na kijana Hassan ambaye alitaka kumuoa Layla. Hawa wamewakilisha kundi lenye asili ya Uarabu. Wahusika hawa walijinasibu kwa Uarabu wao. Haya yanadhihirishwa na wahusika hawa kupitia maongezi yao. Mathalan, wakati Bw. Ahmed akimuelezea Hassan ambaye alileta posa kwa ajili ya bintiye, anasema:

> "…posa ipi? Ile ya yule muhuni?...si yule Mwarabu wa Mwera sijui Fuoni?"(ukurasa 112).

Ahmed ni jina lenye asili ya Kiarabu, historia inaeleza kuwa Waarabu walikuja katika Visiwa vya Zanzibar kwa ajili ya kufanya Biashara. Ndivyo, Bahroon alivyomsawiri Bw. Ahmed, katika *Mungu Hakopeshwi*, anaitoa historia ya wazazi wake kwa kusema:

> "Wazee wetu wote ni wafanyabiashara na hiyo ndiyo sababu kubwa iliyowatoa kwao na kuja bara la Afrika. Lakini watoto wa siku hizi hawataki biashara tuzifanyazo hilo ni tatizo kwao" (Bahroon, 2017: 14).

Katika kundi hili mwandishi amemchora Hafidh mkwe wa Bw. Ahmed kuwa naye ni ni kutoka katika mbari hii hii ya Kiarabu. Mwandishi anabainisha haya kupitia

mazungumzo ya Hafidh na Sada, ambaye alikuwa Mswahili. Sada anasema, "Vipi nitakuamini kirahisi namna hiyo? Kwanza makabila yetu tofauti. Wewe Mwarabu, mimi Mswahili?" (Bahroon, 2017: 175).

### 4.2.3 Kundi la Wahindi

Kundi hili limedhihirishwa na Shafi (1999) katika riwaya yake ya *Vuta N'kuvute* pale alipomchora mhusika Yasmin pamoja na familia yake. Ni kundi la watu wenye kushikilia mila na desturi zao. Kundi hili hupenda kujitenga na kutotaka maingiliano na watu. Migongano mbalimbali imetokea katika jamii inayotokana na kundi hili. Mwandishi, akimuelezea Yasmin. Anasema:

> "Mara tu baada ya kufunja ungo, Yasmin aliozwa mume. Alikuwa mume wa jamii yake ya Ithnashiria…" Shafi (1999: 1).

Nukuu hii inabainisha kuwa Yasmin anatoka katika jamii ya Wahindi. Ithnashiria ni dhehebu mojawapo la Kihindi. Vile vile, kwa familia ya Yasmin wakati mama wa Yasmin anakasirishwa na kitendo cha Yasmin kumkimbia mume wake. Bw. Raza anasema:

> "Umekuja kufenza nini hapa wewe mwenaharamu, umeacha Raza Mombasa umekujisha Zanzibar kufenza uhuni kutilisha sisi aibu. Jamatini vatu ote nazungumza habari yako…" (Shafi, 1999: 38).

Mtindo wa lugha na utamkaji wa maneno ambao mwandishi ameusawiri kwa mhusika huyu unadhihirisha kuwa mhusika anatoka katika kundi la Wahindi. Aidha, neno "Jamatini" linamaanisha sehemu ambayo watu jamii ya Wahindi hukutana kwa ajili ya ibada zao.

### 4.2.4 Kundi la Machotara

Kundi jengine ni lile la machotara au mchanganyiko wa mbari tofauti ambazo zimejitokeza katika riwaya za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*. Kundi hili pia hujulikana kwa jina la *shombe*. Mbari tofauti visiwani (Zanzibar) zinatokana na kuingia kwa ukoloni na kusababisha mchanganyiko wa mbari za Wazungu, Waarabu na Wahindi kuhamia Zanzibar na kutangamana na Waafrika au Waswahili ambao ndio wenyeji Sheriff (2001). Katika riwaya ya *Mungu Hakopeshwi*, mwandishi amebainisha uchotara kupitia mhusika Ahmed mtoto wa Bw. Ahmed, ambaye alikuwa Mwarabu aliyezaa na Bi.Lulu ambaye ni Mswahili. Mhusika Farhat ambaye naye ni chotara. Mwandishi anawabainisha kupitia mazungumzo ya Bi. Khadija, mke wa Bw. Ahmed anagombana na mume wake kwa sababu Bw. Ahmed hataki kumuozesha mwanawe chotara kwa Ahmed. Bi. Khadija anasema:

> Kwani shombe najisi?...Said amemuoa Farhat kabla ya kuondoka Zanzibar…. Unamjua aliyemuoa? Shombe! Mwarabu wa Kisomali. Na ukimuona hata uwekewe kisu cha shingo husemi kama Muarabu. Msomali tiiiiiii.… Sasa utambuwe kuwa ukoo wako ni wa mashombe! (Bahroon, 2017: 216).

Sifa ya taifa la Zanzibar, kama inavyobainishwa katika *Vuta N'kuvute* Shafi (1999:71) ni kuwa ni taifa lenye mchanganyiko wa damu mbalimbali au "mkorogo wa mataifa", yakiwemo Uajemi, Ngazija, Ushihiri, Uhindi, Umanga, Uingereza na Uafrika. Hali hiyo imezaa uchotara wa utamaduni na wakimbari. Bhabha (1994) amebainisha katika nadharia yake ya uchotara kuwa ni ujumuisho wa utamaduni au desturi mbalimbali katika nchi moja. Hali ya kikundi cha watu wenye kuwa na sifa za tamaduni zaidi ya moja. Maingiliano ya mbari tofauti huzaa uchotara wa kitamaduni na uchotara wa kimbari.

Makundi ya kimbari yenye migongano katika riwaya teule za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi* yamezaa athari kuu mbili uchotara wa kiutamaduni na uchotara wa kimbari. Athari zaweza kuwa chanya au hasi. Sababu mojawapo ya kuja kwa wageni wambari ya Kiarabu ni kuwepo kwa ukoloni uliowakaribisha. Katika *Mungu Hakopeshwi*, mwandishi anaelezea kuzuka kwa uchotara kama ifuatavyo:

> "Nijuavyo mimi, nchi ina mchanganyiko wa makabila tofauti wenye asili ya mataifa mengine na hufika kuchanganya nao damu na kuwa na kizazi kipya, lakini bado wanatambuliwa kuwa ni raia halali wanchi hizo. Na wana haki sawa na wale ambao wanaasili za nchini humo!" (ukurasa 11).

Hali hii ni ile aliyoeleza Bhabha (keshatajwa). Utambulisho mpya unazaliwa katika muktadha wa uchotara na uwanda wa tatu. Mtoto wa Bw. Ahmed (Mwarabu) na Bi. Lulu (Mwafrika) aitwaye Ahmed, katika *Mungu Hakopeshwi*, ni chotara au shombe. Kwa kawaida, chotara huyu huwa na sifa za kimwili na kitabia ambazo ni mchanganyiko kutoka pande mbili zilizoungana. Mathalan, muonekano wa Ahmed (chotara) umewafanya wafanyakazi wa Bw. Ahmed waone ni mtu kutoka katika jamii ya Bw. Ahmed pale waliposema, "Ah jamaa moja wale, kama si wa amoo basi ni mtoto wa khaloo. Ndio hao hao wanazunguka humo kwa humo tu" (ukurasa 146). Katika mila za Kiarabu, "Amoo" ni ndugu wa baba, likimaanisha "shangazi" na "Khaloo" ni ndugu wa mama, likimaanisha "Mama mdogo". Muonekano wa Ahmed umesabaisha aonekane kuwa yeye na Bw. Ahemd ni ndugu.

Mtoto wa Denge na Yasmin, au kizazi cha Bukheti na Yasmin katika *Vuta N'kuvute*, ni zao jipya ambalo haliwezi kujiegemeza kwa mbari moja ama ya Kihindi, Kiarabu au Kiafrika pekee. Utambulisho wao ni wa kizazi kipya cha kichotara ambacho ni

matokeo ya uwanda-mpito kama alivyoeleza Bhabha (1994). Kundi hili limezaa uchotara wa namna nyingine kama unavyoonekana katika sehemu inayofuata.

#### 4.2.4.1 Uchotara wa Kiutamaduni

Ushahidi wa uchotara wa kiutamaduni unadhihirishwa katika *Vuta N'kuvute* na Mwajuma ambaye kwa asili ametokea Mikindani na kuja kuishi Unguja sehemu za Donge na kizazi chao kikakua (ukurasa 42). Mwajuma anaonyesha umahiri wa kuimba nyimbo za Kihindi, nyimbo za Kiarabu na nyimbo za Kiswahili (ukurasa 31) hali inayoashiria athari ya uchotara wa mbari tatu za Wahindi, Waarabu na Waswahili huko Unguja. Mwandishi anamuelezea Mwajuma kuwa:

> Humtoka vipande vya nyimbo za kila aina, akiimba huku akifanya kazi zake za nyumbani. Mara huimba nyimbo za Kihindi, mara kipande kidogo cha nyimbo za Kiarabu na kinapomtoka kipande cha nyimbo ya Kiswahili, basi mpita njia yeyote yule aliye ashki lazima atasimama na kumsikiliza (ukurasa 31).

Bila shaka huweza kuimba Kihindi, kisha Kiarabu halafu Kiswahili. Zaidi ya hayo, yanapotokea matumizi ya maneno ya Kiingereza, Kiarabu au Kiswahili katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*, tunathibitishiwa kuwepo kwa uchotara wa lugha ambao ni sehemu ya uchotara wa utamaduni. Uchotara huo unachukuliwa kuwa ni hali chanya kiasi cha kuwaburudisha wasikilizaji na umekuwa sehemu ya utamaduni mpya wa Unguja katika kipindi cha uwanda-mpito. Muktadha huo unazalishwa baada ya watawala na watawaliwa kuishi katika eneo moja na kila mmoja kuonyesha ustadi wake na hivyo kumvutia mwengine Bhabha (1990). Mseto wa kiutamaduni unazaliwa.

Baada ya ukwezaji wa utamaduni wa Kihindi au Kiarabu pekee dhidi ya Uswahili, hali hiyo inavunjwa katika muktadha wa uwanda-mpito Ashcroft (1994 ) na Bhabha

(1994). Umahiri wa tamaduni tofauti unazaa uchotara wa sanaa kwa kizazi kinachokumbwa na maingiliano yanayosababishwa na zao la ukoloni. Mwafrika anajifaharisha na utamaduni wa kutoka katika mataifa mengine. Kwa upande wa Wahindi, Yasmin naye anajifunza tabia na ngoma za Kiswahili kiasi kwamba Shafi anatuambia kuwa Yasmin:

> Aliondokea kuwa mwari mzuri aliyetiwa unyagoni na Mwajuma na unyago aliucheza vilivyo kwani pindi umkutapo benini, kibwebwe amekikaza kiunoni, unaweza kula yamini kwamba yeye si mtoto wa Kihindi aliyezaliwa akakulia Uhindini. Akafunzwa kuwa mbali na Mswahili tokea utotoni kwake. Kwa Wahindi, Yasmin alikuwa asi, aliyevunja miiko yao yote kwa kuchnganyika na Waswahili. Kwa Waswahili, Yasmin alikuwa ni mfano wa jinsi gani watu wa makabila mbalimbali wanaweza kuwa pamoja, wakawa wamoja hata tofauti baina yao zisionekane (Shafi, 1999: 75).

Utamaduni mseto unapozaliwa ni vigumu kujifagharisha na utamaduni mmoja au kubagua desturi ya mbari moja kuwa ni bora kuliko desturi ya mbari nyingine katika muktadha wa uchotara ambapo mtawaliwa na mtawala wapo katika nafasi ya uwanda wa tatu wa kuchangamana Bhabha ( 1994). Si kwa upande wa muziki pekee ambako kunajidhihirisha hali ya mtazamo chanya wa uchotara. Tunaambiwa na mwandishi kuwa ukanda wa Pwani, hususani Zanzibar na Mombasa, utamaduni wa aina mbalimbali kama vile wa vyakula na mapishi ya kigeni na kienyeji ulishashika mizizi. Bukheti alikaribishwa karamu ya chakula na mjomba wake, Bwana Bashiri wa Unguja kwa aina mbalimbali ya mikate yenye asili ya Ngazija, Uajemi na Ushihiri. Katika kusisitiza asili za mikate, Bwana Bashiri alifafanua kama ifuatavyo:

> Kwa mfano, mkate wa mofa na parata, asili yake huko Ushihirini. Nafikiri mkate wa Ajmi, asili yake huko Uajemi, nd’o maana unaitwa wa Ajmi. Na bila shaka wa Kingazija, asili yake huko Ngazija… Hii inaonyesha jinsi Unguja ilivyo mkorogo wa mataifa (Shafi, 1999: 71).

Hali hii inathibitisha mawazo ya Bhabha (1994) kwamba katika nafasi au muktadha wa muungano wa tamaduni mbili au zaidi, kunajitokeza aina ya utamaduni mseto uliobora zaidi.

#### 4.2.4.2 Uchotara wa Kimbari

Tunathibitishiwa na Shafi katika *Vuta N'kuvute*, kuwa taifa la Unguja limegeuka kuwa "Mkorogo wa mataifa", yaani lina uchotara wa kimbari ambao kwa upande mmoja una utangamano wa mbari tofauti ni wenye manufaa kama hayo ya kuwa na ustadi wa mapishi na sanaa tofauti. Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, makundi ya wageni yanawakilishwa na wahusika kama vile Yasmin, Bwana Raza, Gulam, Kulsum, Kermali na Mamdali kwa mbari ya Wahindi. Inspekta Wright anawakilisha kundi la Wazungu.

Kundi au mbari ya Kiarabu haijitokezi waziwazi, lakini kwa majina yao, kama vile Mabruki na Amar Waga, yaelekea ni machotarata wa Kiarabu. Nalo kundi la Waafrika ni kubwa na linawakilishwa na Denge, Mwajuma, Salum, Roger, Faraji, Mambo, Mzee Kiroboto, Chande, Mabalanga, Zanga, Bwana Bashiri, Sukutua, Shihab na Guli (Mngazija). Hivyo, katika *Vuta N'kuvute* tunapambanishiwa mbari tatu waziwazi za Wahindi, Wazungu na Waarabu dhidi ya Waafrika. Makundi haya yapo katika muktadha wa kipindi cha mwisho mwisho cha ukoloni wakati Waafrika wakiwa katika harakati za kujikomboa kutoka katika "makucha ya Serikali ya Bwana Sayyid chini ya himaya ya Muingereza" (Bahroon, 2017*:* 64). Jamii ya Ukoloni kwa mujibu wa Shafi, kuanzia Mombasa hadi Unguja, ilitamalaki mfumo wa kibaguzi na wenye matabaka ya wazi kijamii:

> Siku ile ya wiki ndiyo Wazungu na wale wanaojiweza wanapofanya manunuzi ya mahitaji yao ya wiki nzima. Tofauti na makabwera ambao Jumapili ni siku ya kupumzika na wengine kulala mpaka saa nne wakiyabembeleza maruirui ya pombe ya jana (Shafi, 1999: 11).

Wazungu na Waafrika walikuwa na taratibu za kimaisha zilizotofauti na zenye ubaguzi wa wazi. Hata hivyo, hali ya ubaguzi inadumu katika maeneo machache, kwani kwa kiasi kikubwa uchotara unajijenga taratibu na kuzua uwanda wa tatu.

Hali ya Mkorogo wa mataifa katika kisiwa cha Unguja inaendelea kudhihirishwa na Bahroon katika *Mungu Hakopeshwi* kuwa kuna makundi au mbari tatu za waziwazi zenye Waarabu, Waafrika na Machotara. Kundi linalojinasibisha na mbari ya Kiarabu linaongozwa na Bw. Ahmed, akiwa na mkewe Bi. Khadija, watoto wao Said, Salah, Layla na Zahra. Wengine ni familia ya Bw. Haroub, mkewe Bi. Maimuna, mwana wao Hafidh na ndugu yao Bw. Salim. Mwarabu mwingine ni yule aliyemposa Layla na kukataliwa kwa kipato chake na kazi yake ya kuendesha daladala, aitwaye Hassan. Kundi la Waafrika linawakilishwa na wahusika Bi. Mwanawetu, Bi. Lulu, Sada na wafanyakazi wa Bw. Ahmed, ambao ni Sefu, Khamis, Salumu na Bakari. Kundi la machotara linawakilishwa na Ahmed, ambaye ni chotara wa Kiarabu na Kiafrika na Farhat, ambaye ni chotara wa Kiarabu na Kisomali (Bahroon, 2017*:* 20). Karibu makundi yote au mbari zote za wageni, ukiondoa Wazungu, yaani Wahindi na Waarabu, hujishughulisha zaidi na biashara.

Makundi haya yanabainishwa kupitia wahusika kwa kujinasibisha na kuona ni kikwazo kikubwa katika kuleta utangamano. Haya yanathibitishwa na mhusika Sada mwanamke wa Kiafrika. Mathalan, tunamwona Sada akimbainishia Hafidh mwenye nasaba ya Uarabu kuwa: “Vipi nitakuamini kirahisi namna hiyo? Kwanza, makabila

yetu tofauti. Wewe Mwarabu mimi Mswahili" (ukurasa 175). Kjana wa Kiarabu analikataa jambo hilo kwa kukana: "Nini kabila? Jicho la kupenda halitazami uzuri. Mapenzi majani, popote huota!" (Bahroon, 2017*:* 175).

Kila mbari imekuwa ikijihami kwa upande wake ili kuendelea kudumisha mila zao. Haki za binadamu zinavunjwa kwa kumshurutisha binti wa miaka 17 kuolewa na mzee ili kuwafurahisha wao tu. Kwa upande mmoja, ni kitendo cha kulinda nasaba zao na tabaka la wafanyabiashara wa Kihindi. Kwa upande mwingine ni kuendeleza ubaguzi kwa kung'ang'ania umbari na mfumo dume. Mama yake Yasmin ni zao la mfumo dume badala ya kumtetea binti yake, anaingia katika mkumbo wa kumkandamiza.

Kwa mujibu wa lengo la kwanza la utafiti, data zimedhihirisha makundi mbalimbali ya kimbari ambayo yana migongano katika jamii ya Zanzibar kupitia vitabu teule viwili ambavyo ni *Vuta N'kuvute* pamoja na *Mungu Hakopeshwi*.

Makundi hayo yanathibisha na hoja ya Bhabha (1994) inayosema suala la utambulisho wa watu (waliotawaliwa) haliwezi kutenganishwa na utamaduni wa wale walio watawala. Mfumo wa ukoloni umekuwa ni mfumo ambatani na wenye mwingiliano wa tamaduni mbalimbali. Hoja hii inathibishwa na Fouéré (2015) anasema, mfumo wa kikoloni wa Kiingereza na Kisultani ulijenga matabaka na mgawanyo wa kiutamaduni hususani kati ya Wahindi, Waarabu na Waafrika. Tabaka la wafanyabiashara, hasa wa Kihindi, walijitenga dhidi ya Waafrika katika utangamano wa damu kiasi cha kuendelea kuwa wageni Shafi anathibitisha hayo pale anapolizungumzia tabaka hilo.

## 4.3 Hitimisho

Sura hii imefafanua lengo la kwanza la utafiti ambalo ni kubainisha makundi ya kimbari katika jamii ya Zanzibar ya baada ya ukoloni kupitia riwaya ya Vuta N'kuvute na Mungu Hakopeshwi. Sura hii imebainisha makundi mbali mbali kama kundi la waarabu, kundi la Wahindi na kundi la Machotara. Vilevile katika sura hii mtafiti amebainisha uchotara wa kitamaduni na kimbari ambao umebainika kutokana na makundi yaliyomo katika jamii. Matokeo hayo ya utafiti yanakwenda sambamba na mawazo ya Homi Bhabha (1994) yanayoeleza kwamba utambulisho wa wanajamii hauwezi kutenganishwa na utamaduni wa walio watawala. Hivyo kwa mujibu wa utafiti huu, imebainika kwamba makundi haya yametokana na athari za watawala ambao waliwahi kutawala Zanzibar.

# SURA YA TANO

# KUCHANGANUA AINA ZA MIGONGANO YA KIMBARI YA JAMII YA WAZANZIBARI WA BAADAUKOLONI KATIKA RIWAYA YA VUTA N'KUVUTE NA MUNGU HAKOPESHWI

## 5.1 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia lengo mahususi la pili la utafiti huu ambalo lilihusu kuchanganua aina za migongano ya kimbari ya jamii ya Wazanzibari wa baada ya ukoloni kupitia riwaya teule ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi.* Imebainika kwamba jamii ya Zanzibar ni jamii yenye makundi ya kimbari yenye hisia kinzani za namna tofauti. Utafiti huu umebaini kuwa kumejitokeza kundi la wahamiaji wenye asili ya Kihindi na Kiarabu ambao walijihisi kuwa wao ni bora zidi ya Waafrika. Haya yamesawiriwa na waandishi kupitia kazi hizi kutokana na jamii iliyowazunguka. Hivyo, katika kujibagua, walikumbushana kuwa wao ni wageni tu na hawakubaliki hata kama wana hati ya uraia wa Zanzibar au wamezaliwa Zanzibar. Mawazo hayo yanabainishwa na wahusika wa riwaya hizi. Bw. Ahmed, katika *Mungu Hakopeshwi*. Anaeleza:

> Kwanza nilikuwa raia wa Kenya baadae nikabadilisha uraia nikawa Mtanzania. Sawa na niitwe mgeni maana nina uraia wa passport na si wakuzaliwa, lakini kuna watu hapa tokea wazazi wao wamezaliwa hapa lakini bado wanaitwa wageni sasa raia wa kweli ni nani na ana sifa zipi? (Bahroon, 2017: 153).

Vilevile, Bw. Ahmed analalamika kuona kuwa dola inawabana wao (Waarabu) katika shughuli zao za kiuchumi kutokana na asili yao, jambo linalowafanya kuyumba kiuchumi. Bw. Ahmed anaeleza hali hii kuwa Dola inatutia kitanzi

shingoni na huku ushuru unakuja kuangusha stuli hapo tunabaki na roho zetu (Bahroon, 2017: 13).

Kitendo cha kuingia kwa Ukoloni kunasababisha uhamaji wa makundi ya watu katika mataifa mapya, ambapo wahamiaji hugeuka wakazi wa kudumu katika mazingira mapya huku wakiendelea na ushabiki wa mifumo ya kisiasa na kitamaduni ya nchi walizotokea. Kitendo hicho kinasababisha migongano ya kimbari inayotokana na matokeo ya uchotara wa utamaduni, dini na mbari Bhabha (1994). Moja ya matokeo ya utafiti yanabainisha aina ya migongano katika maeneo ya matabaka ya kijamii, maingiliano ya kindoa, shughuli za kiuchumi, na nafasi za utawala. Tukiliangazia suala la dhana ya matabaka hili linafafanuliwa na Karl Marx kwamba matabaka katika jamii ni pale ambapo baadhi ya wanajamii wanakuwa na kipato kikubwa zaidi kuliko wengine kutokana na unyonyaji unaofanywa na kundi tajiri dhidi ya tabaka masikini (Wamitila, 2002). Aina mbili za migongano ya kimbari imejitokeza katika riwaya hizi mbili, ikiwemo kuzuka kwa *hisia-kinzani* miongoni mwa wananchi. Katika maelezo ya madondoo ndani yake kunaonekana sababu za kutokea migongano na ndani ya sababu hizo ndipo tumepata aina hizo mbili za migongano katika riwaya teule.

## 5.2 Hisia-Kinzani katika Utambulisho

Hisia-kinzani hujitokeza pale ambapo mazingira ya Ubaadakoloni huibua kanuni na tabia mpya za kijamii kiasi cha kuwafanya wahusika kujisikia kuwa na hisia-kinzani. Jamii au kikundi kinaweza kujikuta kikiwa katika mazingira mapya ya kisiasa na kiuchumi kiasi cha kuvurugikiwa kimaono. Bahroon anasisitiza mgongano wa umbari ambao unawanyima fursa ya kujitambua kama raia halali wa Zanzibar kwa

misingi ya nasaba na rangi zao. Athari ya mfumo wa Ukoloni uliosababisha ugeni wao katika bara la Afrika kutokea Ulaya, Uarabuni na Uhindini unajidhihirisha hata mara baada ya kupata uhuru. Bw. Ahmed anaonekana kulalamika kuwa utaifa wake una mashaka na unasababisha hisia-kinzani akilini mwake. Anaeleza:

> Leo sisi tumekuwa wageni hatujulikani ni nani. Basi nani atakuwa mwenye amani ya nafsi wakati hata kwake hapajui wapi? Bara la Afrika hawatutaki na Bara Arabu hawatutambui (Bahroon, 2017:10).

Bw. Ahmed anajihoji juu ya utambulisho wa mbari yake iwapo wenyeji wanashindwa kuwatambua na kuwakubali. Anaendelea kusema kutokana na hisia-kinzani alizonazo kuhusu utambulisho wake:

> Sasa maana ya Mzanzibar sijui nini? Ah! nchi yao wenyewe na serikali yao wenyewe; waache wafanye wapendavyo sisi yetu macho tuone huo mwisho wao watafikia wapi (Bahroon, 2017: 11).

Hali hiyo ya kujihisi mgeni inajenga hisia-kinzani ya "Sisi" dhidi ya "Wao". Bw. Ahmed, katika *Mungu Hakopeshwi*, anamuelezea mwanawe kuhusu maisha yao na ukinzani wa utambulisho wao kwamba tokea mapinduzi tumekuwa tukitazamwa kwa jicho la chuki, siku zote sisi si wema kwao, na mbaya zaidi wanazungumza hadharani chuki walizonazo juu yetu sote . Tunaonekana watu wenye furaha na amani kwa upeo wa macho yao kumbe si hivyo! (Bahroon, 2017:10).

Hali hii ya hisia-kinzani inadhihirishwa na Bw. Ahmed kuwa wao wanajihisi ni wanyonge kwa kubaguliwa na wenyeji Waafrika kwa kutakiwa warudi makwao. Mwandishi Bahroon, kupitia mhusika Bw. Ahmed ameonesha chimbuko la vurugu za maono zinazomkabili yeye kama Mzanzibari mwenye asili ya Uarabuni kuwa:

> Zamani nilikuwa naamini kuwa mimi ni mwananchi halali wa nchi hii. Na nilijivunia kila pahala kuwa mimi ni Mtanzania tena ni

> Mzanzibar. Lakini, kumbe si hivyo wananchi wenywe wanatuita sisi ni wageni na wanatutaka turudi kwetu (ukurasa 153).

Kwa upande wa riwaya ya *Vuta N'kuvute*, Shafi amesawiri jamii ya Kihindi na Kiswahili kwamba wamekuwa na migongano ya kiutabaka ambapo jamii ya Kihindi hujiona kuwa yenyewe ni bora kuliko jamii ya Kiswahili. Anaeleza kwamba:

> Si kama Yasmin alipenda maisha ya kukaa ndani au Mwajuma alipenda kutoka peke yake na kumuacha ndani tu kama kizuka, la hasha. Kila mmoja kati yao alipenda kutoka na kwenda kutembea na mwenzake, lakini Yasmin alifikiri kwamba labda Mwajuma hakupenda kutoka na yeye ili asije akamvunjia starehe zake. Na Mwajuma naye alichelea kumtajia Yasmin mambo ya kwenda kutembea, akifikiri kwamba, kwa vile yeye ni mtoto wa Kihindi, asingelipenda kuonekana amefuatana na mtoto wa Kiswahili kwa hofu, Wahindi wenzake wasije wakamsema (Shafi, 1999: 33).

Katika dondoo hili, tunaoneshwa kwamba upo ubaguzi wa wazi baina ya Waswahili na Wahindi ambao umesababisha wahusika wakuu kuwa na hisia-kinzani katika fikra zao. Hali ya uhatihati (*Inbetweenness*) ya Yasmin imemfanya ajione ni mtu wa mchanganyiko wa Kihindi na Kiafrika. Hawezi kuegemea upande mmoja.

Utabaka unajidhihirisha hata katika kuongozana tu baina ya Mswahili na Mhindi kwamba ni kitu ambacho kinaweza kumfanya Mhindi akatengwa na jamii ya Wahindi wenzake. Haya yanathibitishwa nahisia-kinzani zilizompata Mwajuma. Alichelea kumweleza Yasmin afuatane naye katika randaranda zake akihofu kuwa Mhindi huyu ataonekana na Wahindi wenzake kuwa amefuatana na Mswahili na hivyo kutengwa na jamii hiyo. Naye Yasmin anakuwa nahisia-kinzani juu ya mgongano wa mawazo uliotokana ubaguzi kati ya Wahindi na Waswahili pale anapovunja mwiko wa kuchangamana na mbari nyengine. Anajikuta katika hisia-kinzani anapoamua kuishi na rafiki yake Mwafrika aitwaye Mwajuma. Anajiuliza

maswali mengi kichwani mwake kuwa mpaka lini ataishi kwa Mwajuma, mtu aliyemjua kwa mazungumzo tu na jamaa zake watasema nini wakisikia anaishi Uswahilini na Waafrika (Shafi,1999: 19).

Aina nyingine ya mgongano wa umbari inajitokeza katika kuzuka kwa hisia-kinzani juu ya utambulisho. Baadhi ya wahusika, haswa machotara, wanajikuta katika hisia-kinzani za kujitambuakama raia halali wa Zanzibar kwa misingi ya nasaba na rangi zao. Athari ya mfumo wa ukoloni, uliosababisha ugeni wao katika bara la Afrika kutokea Ulaya, Uarabuni na Uhindini inajidhihirisha hata mara baada ya kupata uhuru watafikia wapi (Bahroon, 2017: 11). Mgongano wa kiutambulisho unaweza kumkumba mtu asitambulike utaifa au mbari yake kiasi cha kujikuta kuwa ni mgeni kote kule anakotokea na katika makazi yake mapya. Hali hii inajitokeza katika kipindi cha uwanda-mpito, kwa mujibu wa Bhabha (1994).

Katika muktadha wa Ubaadaukoloni, aghalabu jamii mpya hupasuka katika vipande au makundi makuu mawili yanayojibainisha kama “wazawa” na makundi ya “wageni”. Kunazuka ufa wa makundi ya “sisi” dhidi ya makundi ya “wao”. Shafi anaisawiri hali ya mpasuko wa kimbari kabla ya uhuru katika jamii ya Wazanzibari ambapo Wahindi wanajitenga na Waafrika. Familia ya Gulam na Kermali wanamwoza binti yao Yasmin kwa Bwana Raza, Muhindi wa dhehebu la Ishnashiri, bila ridhaa yake na kama ilivyo ada ya mbari hiyo. Yasmin kama mwanamke alitarajiwa na watu wa jamii yake kutii amri ya wazee wake ada ya kuwapangia mabinti mtu wa kuwaoa na pia kuolewa ndani ya mbari yao. Mama yake Yasmin anachukua uamuzi wa kumwita binti yake “mwenaharamu” na mhuni anayetia aibu familia yake na Jamatini yote baada ya kuvunja mwiko huo:

> Jamatini vatu ote nazungumuza habari yako, nasema veve siku hizi nafatana na golo. Toka Toka kwenda zako! Mimi sitaki ona uso hata uso yako… (Bahroon, 2017: 38).

Bahroon (2017) naye anatusawiria mpasuko wa kimbari kupitia kwa Bw. Ahmed, Mwarabu mwenye kutetea mfumo wa ubaguzi anapokataa kumuozesha binti yake, Zahra kwa Ahmed, chotara ambaye hakuwa akijua kuwa amemzaa mwenyewe na Bi. Lulu Mwafrika huko Mombasa. Bw. Ahmed anapinga kwa nguvu zote suala la ndoa baina ya watoto wake na mbari nyingine kwa kusema mimi Ahmed Bin Said nikamuozeshe mtoto wangu shombe? (Ukurasa 216). Vile vile, anaweka pingamizi hata kwa mtoto wake wa kiume Said kumwoa chotara wa Kisomali.

Hali ya kubaguana katika muktadha wa Ubaadaukoloni haijitokezi katika riwaya teule pekee za utafiti huu. Katika tamthilia ya *Mfalme Juha* ya Farouk Topan (1971) muktadha wa Ubaadaukoloni uliwaweka wahusika hawa wenye kujinasibisha na mbari tofauti katika mazingira tata yasiyo na uhakika wa kimaisha. Mchanganyiko wa mbari uliopo Zanzibar umesababisha uchotara pamoja na hisia-kinzani kwa wanajamii wenyewe. Hisia-kinzani huwakumba wanajamii juu ya utambulisho wao kutokana na mchanganyiko wa asili zao. Haya yamejitokeza katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* pamoja na *Mungu Hakopeshwi* kama tulivyoona katika maelezo yaliyotangulia.

## 5.3 Hisia-Kinzani katika Ndoa na Mapenzi

Katika riwaya teule, waandishi wamebainisha jinsi baadhi ya wahusika wakuu walivyoasi umbari wao kwa sababu ya mapenzi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Vuta N'kuvute*, mwandishi amemchora mhusika aliyefanya maamuzi ya kupeleka posa

kwa Wahindi.Mhusika wa mbari ya Kiafrika alithubutu kupeleka posa ya kutaka kumwoa Yasmin wa mbari ya Kihindi. Bukheti, aliye Mgunya wa Mombasa au "Golo", kwa mtazamo wa Wahindi, anabaini kuwa si rahisi jambo hilo kutokea. Bukheti anakuwa na hisia-kinzani juu ya kukubaliwa posa yake anamuuliza Yasmin, "Unafikiri Muhindi atasikiliza posa ya Mgunya atokaye Mombasa?" Shafi (1999: 207).

Kihistoria, mbari ya Wahindi katika jamii ya Zanzibar inajulikana kuwa ni yenye misimamo ya kuoana wao kwa wao. Hawataki kuchanganyika na mbari nyingine kwa kuhofia kupotea kwa asili yao. Haya yanathibitishwa na Adam (2014). katika utafiti wake, kutokana na maelezo aliyoyapata baada ya kufanya mahojiano na bwana Mohamed Ravji ambaye ni Mhindi anayeishi Mkunazini Zanzibar. Alisema:

> Unajua, bwana mtafiti, watu wengi, hasa Waswahili, wanashindwa kutuelewa sisi vizuri. Sisi hatuwachukii Waswahili, bali sisi tunapenda kudumisha asili yetu iendelee kuwepo duniani. Sidhani kama kuna mtu ambaye anapenda kuipoteza asili yake. Njia pekee na kubwa katika kutimiza hili ni kuhakikisha kwamba, tunaoana sisi kwa sisi ili kuweza kuidumisha asili hii na tusipofanya hivyo basi sisi tutakwisha. Hii ni sera ambayo, ipo kwa Wahindi wote, wanaoishi katika sehemu mbalimbali duniani na si hapa Tanzania peke yake. Kwangu mimi ninamuona Mswahili kuwa ni mwanadamu na anastahiki kupata heshima zote za kibinadamu, lakini mimi nina utamaduni wangu na yeye ana utamaduni wake (Bahroon , 2017: 74).

Hata hivyo, mwandishi hakusita kubainisha hisia-kinzani zilizojenga woga ambao umetokana na sababu za kihistoria. Mwandishi ameeleza juu ya wazazi wa Bukheti kumshauri mwana wao aoe kutoka katika mbari yake. Haya yanadhihirishwa pale mzazi mmojawapo anaposema ya nini kwenda kutafuta Wahindi, mwanangu? Wewe una jamaa zako chungu nzima (Bahroon, 2017: 226).

Vile vile, kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute*, Shafi amemtumia Gulam, mjomba wa Yasmin, kuwa na mahusiano na mwanamke ambaye hatokani na mbari yake. Kutokana na hisia-kinzani juu ya jamii yake kujua kuwa ameoa nje ya mbari yake, anaamua kufanya siri ili jamii yake ya Kihindi isijue. Shafi anaelezea kuhusu Gulam kuwa anaye mke Mswahili! Tena anaye siku nyingi, amezaa naye watoto wawili… Amemuoa kwa siri.

Kwa upande wa riwaya ya *Mungu Hakopeshwi*, hoja ya hisia-kinzani katika mapenzi na ndoa imedhihirika kwa wahusika wake. Mathalan, Said, mtoto wa Bw. Ahmed, anakuwa na hisia-kinzani juu ya mapenzi yake na Farhat, ambaye ni chotara. Alijua kuwa baba yake asingeweza kumkubalia yeye kuoa mwanamke kutoka katika jamii nyingine. Mwandishi anasema:

> Said alizidi kuchanganyikiwa hakujua hata afanye nini. Kwa hakika alimpenda kweli kweli Farhat na wala hakutaka kumpoteza kwa kitu chochote. Mzee sasa anawaka hashikiki,vipi atathubutu kumueleza juu ya Farhat. Na alijua vyema kuwa vyovyote itakavyokuwa mzee wake asingekubaliana na wazo lake (Bahroon, 2017: 130).

Hisia-kinzani katika ndoa na mapenzi vilevile imebainika kutoka katika familia hii ya Bw. Ahmed. Ni mzee wa Kiarabu mwenye msimamo mkali juu ya kuchanganya familia yake na mbari nyingine. Alipoteza mapenzi kwa watu wake kwa sababu ya msimamo wake huo. Alikimbiwa na mtoto wake Said baada ya kuona hawaelewani mitazamo yao. Pia alipoteza mapenzi kwa kijana wake, Ahmed (ambaye alikuwa ni mwanawe bila ya yeye kujua) ambaye awali alipata bahati ya kupendwa na mzee Ahmed na kuwa naye karibu.

Ahmed alikuwa na hisia-kinzani kuwa vipi yeye atakubaliwa kumuoa Zahra, mtoto wa Kiarabu wa mzee Ahmed? Bi. Khadija naye anakuwa na hisia-kinzani juu ya ndoa ya mtoto wake kwa sababu alijua kuwa mume wake si rahisi akubali. Bi. Khadija anamueleza mume wake:

> Basi hiyo ndio kazi unayoijua wewe,kujisifu tu, 'Ahmed bin Said!' Ndiyo nini? Fikiria maslahi ya watoto badala ya kujitukuza mwenyewe. Mpaka Said amekimbia nyumba kwa ajili yako. Kwani shombe ni najisi? (Shafi, 1999: 216).

Bw.Ahmed akiwa na hisia-kinzani juu ya ndoa hiyo, anaamua kutoa maamuzi huku akiwa amekasirika sana kwa kusema mimi nimeshasema kuwa Ahmed hamuoi Zahra *and that is the final decision.* Bwana Ahmed hasira zilimzidi mpaka kilimtoka Kizungu asijue kakitolea wapi (Bahroon, 2017: 217).

Haya yametokana na vurugu za maono kutokana na wahusika hawa kutaka kufanya mambo ambayo yako kinyume na kaida za jamii zao. Kama anvyoeleza Bhabha (1994) ni rahisi mtu kuwa navurugu za maono pale ambapo anataka kujizoeza kwenye jambo ambalo ni jipya kwake au jamii yake. Kama ambavyo imebainika katika riwaya hizi mbili, waandishi wamewasawiri wahusika wakiwa na hisia-kinzani juu ya yale ambayo walitamani au waliweza kuyafanya.

## 5.4 Hitimisho

Sura hii imeelezea lengo la pili la utafiti huu ambalo ni *kuchanganua aina za migongano ya kimbari ya jamii ya Wazanzibari wa baada ya ukoloni kupitia riwaya teule ya Vuta N'kuvute na Mungu Hakopeshwi.* Mtafiti amefafanua kwamba jamii ya Zanzibar ni jamii yenye makundi ya kimbari yenye hisia kinzani za namna tofauti. Mathalan, hisia kinzani katika utambulisho na hisia kinzani katika mapenzi na ndoa.

Migogoro hii imebuka kutokana na machanganyiko wa mbari tofauti katika jamii hiyo ya Zanzibar. Migongano ya Kimbari inawanyima fursa baadhi ya raia ya kujitambua kama ni raia halali wa Zanzibar kwa sababu tu ya nasaba zao na rangi zao. Vilevile katika sura hii mtafiti ameelezea jinsi migongano ya kimbari ilivyosababisha baadhi wa wanajamii kuasi mbari zao kwa sababu ya mapenzi au ndoa. Haya yote yametokana na vurugu za maono kwa wanajamii juu mila gani au kaida gani azifuate.

# SURA YA SITA

# MIKAKATI YA KULETA UTANGAMANO WA KIMBARI INAYOPENDEKEZWA NA WAANDISHI KATIKA RIWAYA ZA VUTA N'KUVUTE NA MUNGU HAKOPESHWI

## 6.1 Utangulizi

sura hii imechunguza lengo mahususi la tatu la utafiti huu lililohusu kutathmini mikakati ya utangamano wa kimbari inayopendekezwa na waandishi Shafi Adam Shafi na Zainabu Alwi Bahroon katika riwaya zao za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*. Misimamo yao juu ya utangamano wa jamii yao uliokumbwa na migongano ya kimbari katika muktadha wa Ubaadaukoloni na jinsi ulivyojengeka kupitia wahusika wao. Mtafiti alifanya uchunguzi wa kina wa matukio ya wahusika wa riwaya teule pamoja na athari zake katika suala zima la kufanya utangamano na kuachana na ubaguzi. Waandishi wa vitabu teule wanatoa mapendekezo ya namna ya kukabiliana na hali ya ubaguzi na utengamano baina ya mbari tofauti zinazoishi pamoja katika kipindi cha uwanda-mpito cha Ubaadaukoloni katika taifa la Zanzibar.

Mikakati yao inajikita katika matokeo ya jamii mpya ya kichotara kujikuta ikiwa na mabadiliko ya kitabia na utambulisho mpya wa kichotara wa wanajamii wakati wa kipindi cha Ubaadaukoloni (kipindi cha uwanda-mpito) Bhabha (1994). Si hayo tu bali pia uvunjaji wa mipaka ya dini katika mapenzi ya wanajamii wenye asili ya mbari tofauti  pamoja na uvunjaji wa mila za ndoa za kinasaba.

## 6.2 Mabadiliko ya Tabia na Utambulisho Mpya wa Wanajamii

Utambuzi wa uwanda-mpito katika utambulisho wa kimbari unasaidia kupambana na mzimu wa ubaguzi na misuguano ya kimbari kwa kubaini nguvu ya uchotara chanya.

Uzalishaji wa jamii na utambulisho mpya unajitokeza katika jamii ya Zanzibar. Katika kipindi cha uwanda-mpito ambapo misukosuko na hisia-kinzani zinatawala. Masuluhisho yanapatikana katika jamii pale ambapo wanajamii wa mbari moja wanavunja tabia na kutambulisha muonekano mpya wa mbari ya kichotara. Haya yanathibitika kupitia riwaya hizi mbili teule.

Mabadiliko ya tabia ya ubaguzi na utambulisho mpya wa jamii yenye mseto wa mbari inayopuuza mila za kibaguzi, ni moja kati ya athari chanya ya utangamano. Mtafiti amebaini hili kama njia ya kujenga utangamano kwa mujibu wa riwaya teule. Shafi kupitia Yasmin, katika *Vuta N'kuvute* anaamua kuwa jasiri na mwenye maamuzi hata kama maamuzi hayo yatamtia shida za kimwili na umasikini lakini kumpa faraja ya akili, furaha ya moyo na kumuondolea msongo wa mawazo. Wahindi kuishi pamoja na Waswahili ni jambo geni kwani maisha yao ni ya kuishi peke yao. Kujitenga na mbari nyingine imekuwa ni desturi kwao. Mwandishi, kupitia Yasmin ametoa suluhisho la kuleta utangamano kati ya Wahindi na Waswahili. Yasmin anajenga hoja kuwa haoni sababu ya Waafrika na Wahindi kubaguana na kukejeliana. Haya yamebainika katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* Yasmin aliposema:

> Na wanawadharau kwa sababu gani hasa? Wao si watu? Au kwa sababu masikini? Ikiwa wao masikini na mimi nishakuwa masikini, nakula fadhila zao, nakula fadhila za Mwajuma na laiti ingelikuwa si yeye sijui ningeliishi vipi mpaka leo. Ah! Haidhuru na waseme wasemayo, potelea mbali (Shafi, 1999: 38).

Katika riwaya ya *Vuta N'kuvute* kitendo cha Mwajuma (Mswahili) kumkaribisha Yasmin (Mhindi) na kuishi naye baada ya Yasmin kufukuzwa kwao kwa kosa la kulazimishwa kuishi na mume asiyemtaka ni kitendo kinachoashiria hali ya kukubali uchotara na haja ya kuishi pamoja bila ya kubaguana baina ya mbari ambazo

zimejikuta katika uwanda mmoja. Yasmin hakuona sababu ya kufuata amri ya mbari yake ya Wahindi ya kutoingiliana na Waafrika wanaoishi nao kama majirani hivyo aliamua kumfanya Mwajuma shoga yake kwa kuvunja miiko ya Kihindi ya kutoingiliana na Waafrika. Anaeleza:

> Yasmin hana habari kabisa juu ya kusononeka kwa mapenzi kwa Bwana Raza. Mzee huyo alikwishayeyuka kabisa ndani ya mawazo yake na chambilecho maneno ya wazee, mkoko nd’o kwanza ulikuwa ukichanua maua. Yasmin alikuwa kama sasa nd’o kwanza ameiona dunia, dunia ya raha na starehe. Leo huku kesho kule; mara kwenye densi, mara kwenye taarab, mara kwenye beni. Aliondokea kuwa mwari mzuri aliyetiwa unyagoni na Mwajuma na unyago aliucheza vilivyo kwani pindi umkutapo benini, kibwebwe amekikaza kiunoni, unaweza kula yamini kwamba yeye si mtoto wa Kihindi aliyezaliwa akakulia Uhindini, akafunzwa kuwa mbali na Mswahili tokea utotoni kwake. Kwa Wahindi, Yasmin alikuwa asi, aliyevunja mila na miiko yao yote kwa kuchanganyika na Waswahili (Shafi, 1999: 85).

Dondoo hili linaonesha kwamba Yasmin alionekana muasi katika jamii yake kwa kitendo cha yeye kuchanganyika tu na Waswahili. Kitendo cha yeye kuchanganyika tu na Waswahili ni dhambi kubwa isiyosemeka wala isiyosameheka kwa wazazi wake na jamii yote ya Wahindi. Hali hii ndipo mtafiti alipobaini kwamba mwandishi amekuja na suluhilo la mabadiliko ya tabia kwa wanajamii. Wanajamii wanapingana kutokana na mitazamo au mila za jamii zao ambazo zinatokana na athari za Kikoloni. Katika kujenga hoja au suluhisho waandishi husawiri aina ya wahusika mahsusi ilimradi ujumbe uweze kufika.

Mwandishi Shafi alipoulizwa na Diegner (2011) kwa nini amemteua mhusika mwanamke mwenye asili ya Kihindi kama mhusika mkuu katika riwaya yake ya *Vuta N’kuvute* alijibu kama ifuatavyo:

> Nimemchagua Muhindi kuonyesha kama mhusika mkuu kwa kutaka kuondoa ile imani kwamba Wahindi ni watu tofauti na Waswahili au Waswahili ni watu tafauti na Wahindi.… Na ndiyo mpaka mwisho utaona kwamba Yasmin anaolewa, inafanywa sherehe katika ile sherehe wanachanganyika wote, wazazi wake Yasmin na wazazi wake Bukheti, Wahindi na Waswahili wanasherehekea hakuna tena 'Golo' hakuna tena 'Ponjoro'. Sasa nimechukua hii ili... nilitaka kuonyesha uhusiano mzuri wa makabila kwamba unawezekana (Shafi, 1999: 37).

Kwa maneno mengine, amemteua msichana wa Kihindi aitwaye Yasmin na kuyasawiri maisha na mawazo yake yanayopingana na mwiko wa kutokutangamana na mbari nyengine katika jamii ya Zanzibar. Kutokana na suluhisho alilolibainisha, jamii yapaswa kuishi pamoja bila kujali utofauti wa mbari zao. Umbari usiwe sababu ya kuifanya jamii ishindwe kusaidiana, umbari usiwe sababu ya jamii kutopendana na umbari usiwe sababu ya kuwanyima wanajamii uhuru wa kuishi maisha yatakayowapa amani.

Kuzaliwa kwa uchotara ndiko mwanzo wa kutokomeza umbari. Hii ni kutokana na Machotara kutoweza kujinasibu kwa upande mmoja tu, wala kuegemea kwenye mila na desturi za upande mmoja tu. Kwa vile wao ni zao la mbari mbili tofauti hawanabudi kuishi maisha yenye mseto wa mila na desturi mpya. Bhabha (1994) anaeleza kwamba uchotara huingilia mfumo jadi uliokuwepo na kuunda mfumo mseto. Wanajamii wanajikuta wakiwa katika mitazamo yenye tamaduni mseto.

Uamuzi wa Shafi kumtumilia Yasmin katika *Vuta N'kuvute* unafanana na ule wa Bahroon alipomsawiri Said katika *Mungu Hakopeshwi*. Said, kama kijana aliyelelewa katika mbari ya Kiarabu, anakataa msimamo wa baba yake wa kumlazimisha kudumisha mila ya kuoa nasaba ya Kiarabu badala ya chaguo lake

ambalo linatokea kuwa ni binti wa kichotara aitwaye Farhat. Kwa kuona athari zilizojitokeza kwa dada yake Layla, anapinga kuendeleza mila za kuchaguliwa mke asiyemtaka. Aligombana na baba yake kwa kumwambia maneno yasiyofaa kwa mtoto kumwambia mzazi wake. Kusudio la mwandishi ni kubainisha mabadiliko ya tabia, kutoka hali ya utii na kuendeleza mila potofu za kibaguzi kwenda kwenye utangamano kwa kuwaunganisha wanajamii bila kujali mbari zao au hata vipato vyao. Mwandishi amelibainisha hili kama ifuatavyo:

> Utaona wewe, ambaye mpaka umri huo ulionao bado umefumba macho. Yale uliyomfanyia Layla usifikirie kuwa utakuja kunifanyia na mimi. Mimi Said sio Layla! Nitamuoa yule nimpendae mimi na sio unayempenda wewe (Bahroon, 2017: 32).

Uchotara wa kimbari na utamaduni unasababisha kuvunjwa kwa muundo na misingi ya kibaguzi iliyojengeka wakati wa Ukoloni. Muktadha wa uwanda-mpito unavunja “Ugolo” na “Uponjoro” au vuta nikuvute ya “Sisi” na “Wao” katika ngazi ya umbari, mfumo dume na uhafidhina katika jamii. Katika *Mungu Hakopeshwi* (Baharoon, 2017) masuluhisho yanapatikana kupitia mwana wa ndani, ambapo Bw. Ahmed anazikwa na Ahmed. Hafidh, Said na ndugu zake wanasahau tofauti zao na kujirudi. Kifo cha Bw. Ahmed katika *Mungu Hakopeshwi* na harusi ya Yasmin katika *Vuta N’kuvute* ni pande mbili za suluhisho ambalo Shafi na Bahroon wanalitoa kuhusiana na migongano ya kimbari katika jamii ya Zanzibar ya ukoloni na Ubaadaukoloni. Waliokuwa wahusika katika tabaka tawala na tawaliwa wote wanajikuta katika utambulisho mpya wa Mzanzibar mwenye fikra na utamaduni mpya.

Mtafiti anaungana na Mochiwa (2016) katika makala yake yenye kichwa cha habari “Uchotara na ubaguzi wa Kizanzibar” kwa kusema kuwa kuzaliwa ni ajali. Katika

kuzaliwa hakuna mwanadamu aliyechagua jinsia. Hakuna mwanadamu aliyechagua jinsi alivyo leo. Hata kisayansi hakuna uthibitisho unaoweza kueleweka kuwa mtoto anayekuwa tumboni mwa mama yake anaweza kuchagua awe vipi bali binadamu huyo amejikuta akiwa amezaliwa.

Mabadiliko mingine yanaibuliwa kutokana na tabia ya mfumo dume. Ni kutokuwepo na usawa wa kijinsia na kuwepo kwa ubaguzi dhidi ya wanawake na wanaume. Suala la mfumo dume bado limetawala katika jamii na kuwa kama sehemu ya utamaduni, kama unavyoibuliwa katika kazi nyingi za fasihi. Ngaiza (2003) anasema kuwa harakati za kumkomboa mwanamke kutoka katika makucha ya mfumo dume zinashindwa kwenda kwa kasi inayostahiki kwa sababu mfumo dume umeota mizizi kiasi cha kupenya mpaka katika tamaduni na kuwa sehemu muhimu ya utamaduni huo.

Mfumo dume ni tabia isiyofaa ambayo kwa mujibu wa waandishi jamii hainabudi kubadilika. Hii inabainishwa kupitia wahusika katika riwaya hizi teule. Katika *Mungu Hakopeshwi* Bw. Ahmed anawakilisha mfume dume na mbari bora, anakataa bintiye Layla anayemchukulia wa kutoka nasaba bora na yenye kipato kuolewa na kijana Hassan ambaye ni Mwarabu lakini mwenye hali ya kipato kidogo. Mwanae Said, anarithi fikra hizo pale ambapo anakataa dada yake Layla kuchanganya matabaka kwa kipimo cha uwezo. Said anafanya stihizai jambo hilo kwa kusema Layla aolewe na mwendesha daladala?

Mawazo ya kihafidhina ya mfumo dume yanapingwa na mwandishi Bahroon anapomtumia Zahra kubainisha uzindukaji wa tabaka la akina mama

walionyanyaswa kwa muda mrefu. Zahra anajenga hoja kuwa mwanamke anahaki ya kuchagua mchumba kama ilivyo kwa mwanaume (Bahroon, 2017: 109). Bi. Khadija anaonyesha kukerwa na tabia hiyo ya mfumo dume na kuamua kufanya mabadiliko. Vile vile, mabadiliko ya tabia pamoja na utambulisho mpya wa wanajamii unadhihirishwa na Bahroon kwa kuvunja nguvu ya mfumo dume kupitia mhusika Bi. Khadija katika harakati za kufanikisha ndoa ya Ahmed na bintiye Zahra kwa kuivunja amri ya Bw. Ahmed ya kukataa ndoa hiyo isifanyike kwa misingi ya unasaba hafifu na uchotara wa Ahmed. Bi. Khadija anaamua kuvunja kanuni za nyumba ya Bw. Ahmed kwa kusema:

> Lakini sikiliza nikwambie Ahmed! Usijaribu kuubadilisha mkondo wa maji uwachukulie vile unavyokwenda ama patakuja kutokea machafuko. Imani, huruma, upendo na utii wa mwanamke usichukuliwe kuwa ndio udhaifu wake ukifikria hivyo utaangamia. Mwache mwanamke vile alivyo kwani atakuja kuwa hatari anapobadilika (Bahroon, 2017: 137).

Bahroon anaendelea kujenga jamii mpya kupitia Bi. Khadija kwa kuhimiza mabadiliko ya tabia na utambulisho mpya wa jamii. Jamii inahitaji uhuru wa maamuzi yatakayowapa faraja. Haya yanathibitishwa na kauli hii kwamba hivi wewe Ahmed ana kasoro gani hata leo ukatae kumuoza mwanao. …kama umasikini kama unavyojidai hii si sababu ya msingi. Wewe uliponioa mimi ulikuwa una nini?... na huyo tajiri uliyempa mwanao matokeo yake yamekuwa nini? Basi kwa nini husomi? Bahroon (2017: 216).

Bi. Khadija anavunja ukimya kwa kumueleza ukweli Bw. Ahmed. Tabia hii inamshangaza mume wake kwani hakuwa mwanamke mwenye tabia hiyo. Bi. Khadija alikuwa ni mwanamke maridhia na mwenye kumsikiliza mume wake.

Mwandishi ameonyesha mabadiliko katika kutetea haki. Mfumo dume wa Bw. Ahmed ambao kwake yeye ndio aliona ni heshima unafikia kikomo. Nukuu ifuatayo inathibitisha hoja hii:

> Ama kweli watoto ni fitna kubwa. Leo hii unathubutu kuzungumza na mimi vile upendavyo kwa ajili ya watoto tu? Iko wapi ile heshima yako juu yangu? (Bahroon, 2017: 217).

Katika kubainisha utambulisho wa jamii mpya, Bahroon anasisitiza kuwa wanawake hawana budi kuamka kujitafutia haki zao wanazokandamizwa dhidi ya mfumo dume uliopo katika jamii zao. Ujumbe wa Bahroon ni kuwa "Mwanamke anaweza kufanya chochote anapoamua".

## 6.3 Mapenzi Yasiyo na Mpaka wa Kimbari

Kila mtunzi anauwezo wakuwajengea wahusika wake haiba mahususi na namna yao ya kukabiliana na changamoto za kimaisha. Wahusika hao hujengewa matendo tofauti wakati wa kuishi katika hali ya amani au hali ya ukoloni. Kutokana na kuwa jamii mbalimbali zimejikuta zikiwa chini ya utawala wa mwingine kiutamaduni katika kipindi cha ukoloni waandishi huunda wahusika wao na njia anuai za kukabiliana na changamoto za Kiubaadaukoloni Young (2001). Haya yanathibitika kupitia wahusika katika riwaya hizi teule ambazo waandishi wamewasawiri wahusika wao kwa lengo la kufukia dhamira waliyoikusudia.

Mtafiti amebaini hoja ya mapenzi yasiyo na mpaka wa kimbari kama njia nyingine iliyoibuliwa na mwandishi katika kuleta utangamano kutokana na migongano ya kimbari katika jamii ya Zanzibar ya baada ya ukoloni. Katika kuibua hoja hii, Bahroon amemchora Hafidh (Muarabu) katika shughuli zake za biashara ya dhahabu

akiwa na tabia ya kubadilisha wanawake wa kila aina bila ya kujali mbari, nasaba, hadhi, umri au ukoo. Bhabha (1996) anaeleza kuwa nafasi ya uwanda-mpito inayozalisha uzazi wa “Machotara” au “Mashombe” kwa kutangamana kimwili baina ya wapenzi wa mbari tofauti. Kwa mujibu wa Bahroon, mhusika Hafidh anasawiriwa katika hali hiyo kwa kuwa na mahusiano na watu tofauti bila kujali lolote. Katika kuibua hoja hii ya mapenzi yasiyo na mpaka wa mbari wala dini, Hafidh anasema:

> Nini kabila? Jicho la kabila halitazami uzuri. Mapenzi majani, popote huota! Hata, Mungu mwenyewe anasema ‘nimewaumba wanadamu kwa makabila tofauti ili watambuane na mbora mbele ya Mwenyezi Mungu ni mcha Mungu’…basi kwa nini utofauti wa makabila yetu iwe ndio kikwazo cha sisi kuungana… (Bahroon, 2017: 177).

Mwandishi anamuelezea Hafidh kuwa ni mwenye tabia ya kumpenda kila anaemuona, si kwasababu alikuwa na lengo la kuoa, huku ni kuvunja mipaka ya dini. Hafidh ni Muislamu na dini yake inakataza mahusiano ya namna hii ya kuwa na mahusiano ya nje ya ndoa. Vilevile, familia yake ilimchagulia mke kutoka katika mbari yake ili kuenzi mila zao. Jambo hilo halikukubaliwa kwa Hafidh. Mwandishi anasema:

> Hafidh alikubali kuingia baada ya kuambiwa kuwa wazazi hawakuwepo, lakini pia alikuwa anataka kumuona shoga. Alijipa moyo kuwa baada ya Sada itakuwa zamu yake (ukurasa 177).

Mwandishi ameendelea kubainisha mkakati huu wa kiutangamano kupitia mhusika mwingine, Said. Katika *Mungu Hakopeshwi*, anagombana na baba yake kiasi cha kutoleana maneno makali pale ambapo Said anamkatalia baba yake kumuoa mke wa nasaba yake na badala yake kujichagulia chotara. Bahroon amewasawiri wahusika katika kufikisha ujumbe kwamba kizazi cha sasa hakijiegemezi kwenye mila za wazazi wao ambazo zimetokana na athari za kikoloni. Vilevile, mila na tamaduni

hizo zimesababisha migongano mbalimbali katika jamii. Katika kuleta utangamano. Bahroon amependekeza hayo ili jamii iweze kuepukana na migogora na hatimaye iweze kuendelea kiuchumi, kijamii na hata kisiasa.

Kwa upande mwingine, katika riwaya ya Shafi ya *Vuta N'kuvute*, mwandishi amemsawiri Yasmin kuwa kivutio cha wanaume wambari zote. Wahindi, Waafrika na machotara kama ua la Asumini humnukisha yetoye yule mwenye pua na uwezo wakutambua harufu nzuri. Yasmin anaolewa na Muhindi, Chotara na Mgunya katika ndoa ya Kiislamu (ukurasa 144-145). Baada ya kuachana na mume wake wa kwanza katika ndoa ya Kiislamu, anakaa eda kwa mila na desturi za Kiislamu. Hivyo, Uislamu unampa tiketi ya kuwa na mahusiano ya kindoa na mwanaume mwingine wa mbari tofauti.

Yasmin anaufuata moyo wake unavyotaka kwa kumpenda amtakaye na sio kulazimishwa. Badala ya kuingia katika ndoa ya kulazimishwa, anautumia uhuru wake kumchagua ampendaye na kuwa na mapenzi ya dhati bila ya kujali mbari zao au ukaribu wa nasaba. Katika hali hiyo, mwandishi anamsawiri Yasmin akiwa na uzuri na mvuto ambao unavunja utabaka. Mwandishi anaendelea kutoa suluhisho la utangamano kwa kubainisha hoja ya mapenzi yasiyo na mpaka wa mbari. Haya yanathibitika kupitia mjomba wa Yasmin (Gulam) ambaye alifunga ndoa na Mswahili kwa siri ili familia yake isijue. Mwandishi anaeleza:

> Anaye mke Mswahili! Tena anaye siku nyingi, amezaa naye watoto wawili wa kiume tena wakubwa sasa. Amemwoa kwa siri. Ni siri hajui mtu yeyote. Yuko Vikokotoni (Shafi, 2017: 224).

Hivyo, mapenzi hayana mipaka. Mapenzi yamesababisha kutangamana na Waswahili na kuwa familia yake nyingine. Jamii inamkubali Yasmin juu ya kuwa na

moyo mkunjufu usio na ubaguzi wala chuki. Waafrika wanamtambua hivyo na kumbainishia waziwazi:

> Wewe mwenzetu Yasmin. Umeshatufanyia mengi katika kuendeleza matumaini yetu. Kumbuka jinsi ulivyoshiriki. Kumbuka jinsi ulivyotusaidia kuwababaisha polisi …Wewe ni mmoja wetu usiogope wala usihuzunike... Kumbuka hayo yote pamoja na pendo lako kwa ndugu yetu Denge (ukurasa 203).

Kinachompelekea kuingia katika harakati za kuwakomboa waliowengi na kuupinga utawala wa kibaguzi ni mapenzi yasiyo na mipaka. Mapenzi yamechukua nafasi kubwa katika maudhui ya riwaya ya *Vuta N'kuvute* ya Shafi Adam Shafi. Mwandishi Shafi amewachukua wasomaji wake katika bahari ya mapenzi ambapo si tu ameelezea namna mapenzi yanavyojitokeza baina ya wapendanao bila ya kujali mbari au itikadi zao bali pia ameyachukua mapenzi kama kivunja mipaka.

Katika *Vuta N'kuvute* wahusika Shihab, Dhahir na watoto wa kichotara wa Gulam na Ahmed, na Farhat katika *Mungu Hakopeshwi* wanakuwa ni ushahidi wa zao la mapenzi ya kimbari yanayokiuka kanuni za kidini na kimila za mahusiano nje ya ndoa. Yasmin katika *Vuta N'kuvute*, anayakataa matakwa ya jamaa zake Waithnashiria ya kumlazimisha aolewe na mume mzee wa nasaba yake na kuamua kutoroka na kuishi na Waafrika. Anakuja kuolewa na Bukheti ambaye ni Mgunya na kuzaa na Denge ambaye ni Mwafrika na pia kutafuta suluhisho linalokuja kujulikana baadaye kuwa vinara wa uhafidhina ndio watuhumiwa namba moja wa utangamano wanaoupiga vita. Kwa siri wanajenga utangamano kwa kuwa na wapenzi wa Kiafrika Bwana Gulam na Bw. Ahmed. Kidhahiri wanapigania uhafidhina wa mbari ya Kiarabu na Kihindi. Hivyo, Shafi na Bahroon wanauumbua mfumo wa uhafidhina wakutaka kuikweza nasaba iliyokwisha changanyika na kuwa jamii mpya.

Kizazi kipya kinawaona wazazi wao ambao bado wanang'ang'ania tabia na desturi za kihafidhina, kama vile za kuwachagulia watoto wao wake wa kuoa kuwa ni kitendo kilichopitwa na wakati. Kitendo kinacho dhihirisha ugumu wa kufikiri. Zahra anawakilisha kizazi kipya chenye fikra mpya na Layla anabakishwa njia panda na hisia-kinzani ambapo kwa upande mmoja anakubaliana na mawazo ya nduguye. Kwa upande wa pili, anahisi kuwa bado nguvu za ubabe wa wazazi wake zinatamalaki hivyo, hana budi kufuata. Wazazi wetu ndio hawa! Wagumu wa kufahamu, kila kitu wafanye kwa amri zao tu. .

Mapenzi hayana mipaka. Shafi Adam Shafi analithibitisha jambo hilo kupitia riwaya yake ya *Vuta N'kuvute*. Hata pale ambapo kuna vikwazo, miiko na desturi ya kutoingiliana kindoa au kimapenzi kwa jamii au mbari tofauti ambazo huweza kujitenga kimakazi, kiitikadi, kitabaka na kifamilia bado mapenzi yanaweza kuvunja mipaka hiyo. Utamaduni si jambo lenye kubaki katika hali ileile isiyo ya mabadiliko. Utamaduni ni mchakato wa mabadiliko ambapo hakuna utamaduni wenye hali ya umenyu. Mbari ya Kiashneri inakumbwa na mabadiliko yanayoletwa na Gulam kwa siri na Yasmin kwa dhahiri. Mwiko wa kutokuoleana unavunjwa kivitendo na Yasmin. Taasisi ya ndoa ya Kiislamu inalikaribisha tendo la kuoana baina ya mbari tofauti chini ya misingi ya Uislamu. Kufuatia ndoa ya Yasmin na Bukheti jamii ya Zanzibar inazaliwa upya.  Dhambi ya chuki inasafishwa na ndoa yenye baraka za wazazi na ndugu wa pande zote mbili.

### 6.4 Uvunjaji wa Mila za Ndoa za Kinasaba

Ndoa za Yasmin zinathibitisha kuondoka kwa matabaka au kuunganisha mbari za "Ugolo" na "Uponjoro" kuashiria suluhisho la utangamano wa kimbari. Mandhari ya

Unguja, Mombasa na Tanga zinahusishwa na mwandishi katika suluhisho la migongano ya kimbari. Madhehebu ya Kiaethnasheri, Kisunni na hata Kikomunisti yanashirikishwa katika mahusiano ya Yasmin na wanaume wanne tofauti. Hakuna anayemkubalia matendo hayo katika jamii na ukoo wake lakini anapambana hadi mwishoni kulazimisha ndoa ya Kiislamu baina yake na Mwafrika Bukheti ambapo inadhihirika pia kuwa mjomba wake ameoa mke wa Kiafrika na ana watoto wawili. Anakubali kupoteza hadhi yake ya kitabaka na kuishi na walio chini yake ili kuufurahisha moyo wake na kupingana na uonevu.

Kitendo cha kuivunja ndoa ya kindugu kinampandisha Yasmin katika jamii yake badala ya kumshusha. Prager (2014) katika *The Dilemmas of Intimacy: Conceptualization, Assessment, and Treatment* anaelezea kuwa mtu anaposhindwa kukidhi haja ya matamanio yake katika mahusiano ya kimapenzi, hujitafutia uhuru wake. Watu wa aina hii hujihisi kwamba wakiwa katika uhusiano wa kindoa huwa katika hali ya ufungwa. Yasmin alijichukulia kuwa nimfungwa wa ndoa ya Bwana Raza katika *Vuta N'kuvute*. Hakujali utajiri wake, bali aliamua kufuata kile ambacho roho yake inapenda. Yasmin alimpenda Denge na kubahatika kupata mtoto na Bukheti naye alimpenda kwa dhati mpaka kukubali kufunga nae ndoa.

Zainab Bahroon, kupitia Bi. Khadija, katika *Mungu Hakopeshwi* anatumia fursa ya kutoa mawaidha yenye kulenga kuleta utangamano wa kimbari pale Ahmed alipojenga hoja kuwa ni vigumu yeye mtu wa nasaba na daraja hafifu kuchanganya damu na binti wa nasaba ya Kiarabu na wa daraja la juu na tajiri. Basi vipi niote kuchanganya damu na ukoo mkubwa kama huu. Bi. Khadija, hali ya kuwa yeye ni Mzanzibari mwenye asili ya Kiarabu na mwenye kutoka katika nasaba ya

wafanyabiashara, anaivunja fikra hiyo ya kijana masikini na chotara, akisema: “Ahmed usiwe mjinga kiasi hicho, mali na nasaba ya mtu si misingi ya ndoa. Unataka kuniambia wale waliozaliwa nje ya ndoa ama maskini hawana nafasi ya kuoa?”. Ahmed anapoendelea kukaidi hoja hiyo kwa kigezo cha watu wanasaizi zao, Bi. Khadija anampa somo Ahmed na kizazi kizima cha sasa kuwa mwanamke hahitaji chochote kwa mumewe isipokuwa mapenzi ya kweli yenye uaminifu juu yake na amali. Huu ni msimamo wa Bahroon kuwa mapenzi na kujaliwa ndicho kiini cha ndoa. Katika kulipendekeza suluhisho Bahroon kupitia mhusika Bw. Ahmed anaonyesha usambamba waumbari na uchotara wa Barack Obama kuwa hauna tofauti na ule wa machotara wa Kizanzibar anasema;

> Mwangalie Barack Obama. Baba yake ni Mkenya kabisaa, lakini amekuwa yeye ni rais halali wa Marekani na kwa kulitihibitisha hilo amekuwa ni raisi wa nchi hiyo, ambae amevunja rekodi kuwa Mmarekani mweusi kuongoza taifa hilo. Lakini huku kwetu ni tofauti kabisaa, yana mwisho (Bahroon, 2017: 11).

Kitendo cha Said kutaka kuoa mke wa kumchagua mwenyewe kinatafasiriwa na Bw. Ahmed kama kitendo cha kutaka kumuundia “matabaka” ndani ya nyumba yake. “Usitake kuniundia matabaka kwenye nyumba yangu. Baki na imani yako peke yako usitafute wafuasi” (ukurasa 79). Lakini Bw. Ahmed anajisahau kuwa tayari tabaka jipya limekwishaundwa na tayari wafuasi wake wamekwisha imarika akiwemo mkewe Bi. Khadija, Ahmed, Said na Zahra. Mwandishi anapinga wazo la kijana kuchaguliwa mume au mke na wazazi wake. Hoja anayoijenga kupitia Zahra ni kuwa imani ya wazazi ni kuwa heshima ni kuwachagulia watoto wao wachumba wa kuwaoa. Zamani wao watoto wanawake walikuwa wanafichwa chini ya mivungu.

Hakuna anayejali hisia za mtoto wa kike. Sasa maisha yamebadilika na watoto wa kike wanatoka nje wanakutana na watu tofauti.

Mawazo ya Shafi naBahroon yanaakisi dhana ya uwanda-mpito inayoangazia nafasi ya mabadiliko au mipaka (Gennep, 1960). Katika kitabu chake cha *Location of Culture* (1994) Bhabha anaitaja dhana ya mpito yenye sifa za utata, uchotara na mabadiliko. Eneo ambalo mabadiliko ya kitamaduni hujitokeza na mazingira hayo huweza kuzua jambo jipya. Hali ya mpito hawakumba watu au kikundi ambacho kipo katika ati ati na wasiojielewa wako katika hatua ipi ya maendeleo. Watu au kikundi kinachojisikia kutengwa bila utambulisho maalum au nguvu ya ushawishi Thomassen (2006).

Pamoja na kujitokeza kwa wingi kwa suala la migongano ya kimbari, pamoja na jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujaribu kulitatua suala la maingiliano ya kindoa baina ya mbari tofauti jamii ya Zanzibar inaibuliwa kama jukwaa ambalo suala la ndoa na maingiliano ya kimapenzi baina ya wanajamii wa mbari tofauti limekuwa halikwepeki. Kwa upande wa serikali, inaweza kupitisha sheria ya kutokubaguana lakini nguvu ya dini inaweza kulitatua tatizo hilo ambapo ndoa ya Waislamu wa Kishia na Kiafrika huweza kujitokeza. Katika miji ya pwani kama vile Unguja, Dar es Salaam, Tanga, Lamu na Malindi kumejitokeza mifano mbalimbali ya maingiliano baina ya Wahindi na Waislamu wa Kiafrika.  Utafiti wa Adam (2014) na Mbogoni (2018) na kazi za Shafi (1999) na Bahroon (2017) ni ushahidi wa suala la maingiliano baina ya Wahindi, Waarabu na Waafrika lilivyo mtambuka katika muktadha wa Ubaadaukoloni au uwanda-mpito (Bhabha, 1994).

## 6.5 Hitimisho

Katika sura hii, uwasilishaji, mjadala na uchambuzi wa data umefanyika na kufanya utafiti huu kukamilika. Lengo mahsusi la tatu ya utafiti huu yamekamilishwa. Lengo hilo linahusu kutathmini mikakati ya utangamano wa kimbari inayopendekezwa na waandishi Shafi Adam Shafi na Zainabu Alwi Bahroon katika riwaya zao za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi*. Mikakati ya waandishi imejikita katika matokeo ya jamii mpya ya kichotara kujikuta ikiwa na mabadiliko ya kitabia na utambulisho mpya wa kichotara wa wanajamii wakati wa kipindi cha Ubaadaukoloni. Katika sura inayofuata inahusu muhtasari, hitimisho na mapendekezo.

# SURA YA SABA

# MUHTASARI, MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

## 7.1 Utangulizi

Sura hii ya saba inahusu muhtasari wa utafiti, utoshelevu wa nadharia iliyotumika katika uchambuzi na mjadala wa data zilizowasilishwa matokeo ya utafiti na mchango wa utafiti. Pia kuna mapendekezo na hitimisho la utafiti.

## 7.2 Utoshelevu wa Nadharia

Nadharia ya Ubaadaukoloni ilitumika katika uchambuzi na mjadala wa data za utafiti huu. Nadharia hiyo ilimuongoza mtafiti kuwaweka waandishi wa riwaya zilizochunguzwa katika ulimwengu wao wa kawaida katika uchambuzi na uhakiki wa data. Waandishi wa vitabu teule walitazamwa namna walivyoyachunguza masuala yanayohusu migongano ya kimbari katika jamii za Zanzibar na kuyaweka kama yalivyo kwa kurejelea kazi zao. Riwaya zilizorejelewa za *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi* zilihakikiwa moja kwa moja kwa kuzingatia muktadha wa uandishi. Nadharia ilimruhusu mtafiti kuchunguza matokeo ya migongano ya kimbari Visiwani Zanzibar kupitia vitabu teule.

## 7.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga 'Kuchunguza Migongano ya Kimbari katika Muktadha wa Zanzibar ya Baadaukoloni kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi'*. Utafiti uliongozwa na malengo mahsusi matatu. Mjadala wa data zilizowasilishwa uliongozwa na nadharia ya Ubaadaukoloni. Matokeo ya mjadala wa data za uchunguzi uliofanyika yameelezwa katika katika sura hii.

Lengo mahsusi la kwanza lilihusu kubainisha makundi ya kimbari yanayoonekana katika jamii ya Zanzibar ya Baadaukoloni kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi.* Tasinifu hii imebaini kuwa suala la matabaka ya kimbari katika jamii ya Zanzibar kiasi kwamba lilikuwepo na baada ya mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. Suala hilo limeoneshwa kuwa lilikuwepo na bado linaendelea na kujidhihirisha katika sura tofauti zenye mshabaha unaofanana. Licha ya kuwa riwaya teule zilizopishana kwa takribani miongo miwili, zinadhihirisha uzito wa suala la nani ni raia wa Zanzibar kwa kurejelea misingi ya kikatiba, kisiasa na kiutamaduni. Waandishi wote wameonesha dhana ya uzalendo na utaifa kwa kuwa wanapigania kuwepo kwa usawa. Makundi mapya ya viongozi wachache nayo yamekuwa sehemu ya matabaka yanayonufaika wakifuatiwa na tabaka la wafanyabiashara ambao wanakutana na kundi kubwa la wasionacho huko mitaani. Makazi ya miji yanayoakisi matabaka kwa rangi, uwezo, umbari, dini, utaalamu, kazi, ujuzi, uono, ulimwengu, mahusiano, matakwa na haki ya ulinzi wa raia na mali zao yapo chini ya serikali na vyombo vyake.

Lengo mahsusi la pili lilihusu kuchanganua aina za migongano ya kimbari ya jamii ya Wazanzibari wa Baadaukoloni kupitia riwaya ya *Vuta N'kuvute* na *Mungu Hakopeshwi.* Lengo la tatu lilihusu kutathmini mikakati ya utangamano wa kimbari inayopendekezwa na waandishi wa riwaya ya teule. Utafiti huu umebaini kwamba makundi mbalimbali ambayo yamo katika jamii ya Zanzibar ya baadaukoloni kama vile ya Waarabu, Wahindi, Wangazija na kundi la Machotara. Mtafiti amebainisha aina mbalimbali za migongano iliyosababishwa na utofauti wa kimbari katika jamii ya Zanzibar. Mathalan, hisia kinzani juu ya utambulisho wa wanajamii ndoa za

kulazimisha na familia kutengana. Kwa upande wa mwingine, mtafiti alifanya tathmini juu ya masuluhisho yaliyopendekezwa na waandishi katika kuleta utangamano wa jamii uliotokana na migongano ya kimbari ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa mabadiliko ya tabia za wanajamii na ujengaji wa jamii mpya.

## 7.4 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umegundua kuwa riwaya teule zilizochunguzwa ni mojawapo ya nyenzo zinazoeleza wazi namna dhana ya umbari na athari zake zilivyojiimarisha katika jamii za Zanzibar. Utafiti huu umebaini kuwa jamii za Visiwani Zanzibar haziwezi kukwepa uchotara wa kitamaduni uliotokana na kuingia kwa Ukoloni wa Mwingereza na Usultani wa Kiarabu. Mwingiliano huo ulisababisha jamii ya Wazanzibari kugeuka na kuwa jamii ya Kichotara kwa vizazi na utamaduni wake. Mchango mpya wa utafiti huu kwa mujibu wa matokeo ya utafiti kutoka katika riwaya teule ni kwamba licha ya kuwepo kwa migongano ya kimbari lakini bado kuna tumaini la kuwepo kwa utangamano thabiti baina ya wanajamii wanaojihisi kuwa wao ni wageni dhidi ya wenyeji wa Visiwani Zanzibar.

## 7.5 Mapendekezo

Utafiti umeangazia suala muhimu sana kwa maslahi ya kizazi kipya. Hali hii ni kutokana na mabadiliko ya kiulimwengu ambayo hutokea katika jamii mbalimbali na kusababisha migogoro ambayo athari yake ni kubwa kwa jamii. Baada ya utafiti huu, mtafiti anapendekeza wanafasihi kuendelea kulielezea suala hili katika kazi zao kwa kuangazia kazi nyingine za fasihi kwa lengo la kuifahamisha jamii na kuibadilisha juu ya dhana mbaya zitokanazo na suala la umbari.

Pili, mbari tofautitofauti katika jamii ya Zanzibar ni utajiri mkubwa ambao unachagiza katika maendeleo yakiwemo ya uchumi kupitia utalii. Hivyo tunapendekeza mbari hizo zienziwe na kupewa fursa sawa katika nyanja mbalimbali ili kukuza utangamano wa kijamii miongoni mwa Wazanzibar.

Tatu, tunapendekeza mikakati madhubuti zaidi ibuniwe kwa lengo la kujenga jamii imara na yenye mshikamano licha ya mbari tofautitofauti na kutoyumbishwa na jambo ama tukio lolote liwe la kisiasa ama kijamii. Watunzi wa kazi za fasihi wanashauriwa kuendelea kutunga na kuandaa kazi zenye mkondo huo wa kuimarisha mahusiano ya mbari katika jamii ya Zanzibar.

## 7.6 Hitimisho

Kwa jumla utafiti huu umefanikiwa kubainisha makundi ya kimbari kama yalivyojitokeza katika riwaya teule ambayo kundi la Waafrika au Waswahili, kundi la Waarabu, kundi la Wahindi na kundi la Machotara. Kwa upande wa aina za mbari tumepata mbili ambazo ni mbari za hisia-kinzani katika utambulisho na hisia-kinzani katika ndoa na mapenzi. Pia, tumefanikiwa kubainisha mikakati ya kutatua changamoto za kimbari ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya tabia na utambulisho mpya wa wanajamii, mapenzi yasiyokuwa na mpaka wa kimbari na uvunjaji wa mila za kinasaba. Jamii ya Wazanzibar ni ya kipekee sana kutokana na uwepo wa mbari mbalimbali za makundi ya wanajamii jambo ambalo likitazamwa kwa umakini na kupewa nafai stahiki katika sera na mipango ya serikali linaweza kuchangia sana katika kuvutia utalii na kukuza uchumi wa Zanzibar. Hii ni kwa sababu Zanzibar haina uwanda mpana wa rasilimali asilia na hivyo uwepo wa umbari ni miongoni wa rasilimali muhimu ya kutumiwa katika kukuza uchumi wa Zanzibar.

# MAREJELEO

Abussamen, A. K., and Neimneh, S. S. (2018). Chinua Achebe and post-colonial ambivalence: gratitude and revenge in *Things Fall Apart*, *No Longer at Ease*, and *Arrow of God*. *American journal of creative education*,1(1), 1-12.

Adam, M. (Ed.) (2015). *Indian Africa: Minorities of Indian-Pakistani origin in Eastern Africa*. Dar es Salaam: Mkuki na nyota publishers.

Adam, O. (2014). Kuchunguza dhamira za kijamii na kiutamaduni katika riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka *Kuli* na *Vuta N'kuvute*. Tasinifu ya uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania,Tanzania.

Ali, J. A. E. (2017). Kuchunguza dhamira katika riwaya ya Kiu ya Mohamed Suleiman Mohamed. Tasinifu ya umahiri (Hiajachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tanzania.

Ashcroft, B. (1994). Interpolation and post-colonial agency. *New literatures review*, 28(29), 176-189.

Ashcroft, B., Griffiths, G.& Tiffin, H. (Eds.). (2004). *Key concepts in post-colonial studies*. London & New York: Routledge.

Bahroon, Z. (2017). *Mungu Hakopeshwi*. Dar es Salaam: Mkuki na nyota publishers.

Baradyana, J. S and Ame, A. M (2005). *Quntitative tecniques for business*. Dar es Salaam: Mkuki na nyota publisher Ltd.

Bhabha, H. (1990). *Nation and narration*. London: Routledge.

Bhabha, H. (1994). *The Location of culture*. New York: Routledge.

Bhabha, H. (1996). Culture's in between: In S. Hall & P. du Gay (Eds.), Questions of cultural identity.(pp. 53-60). London: SagePublication.

Biersteker, A. (2012). War of words, war of stones: Racial thought and violence in colonial Zanzibar (Review of the book) . *Research in African literatures*, 43(2), 190.

Chachage, S. (1996). *Environmental aid and politics in Zanzibar.* Dar es Salaam: Dar es Salaam university press.

Cohen, L., Manion, L., & Morriso, K. (2000). *Research methods in education* (5th ed). London: Routledge

Cook, D.& Okenimke, M. (1987). *Ngugi wa Thiong'o: An exploration of his writings.* London: Heinemann.

Diegner, L. (2011). "Mazungumzo na Adam Shafi juu ya uandishi wake wa riwaya," katika, *Swahili Forum* 18: 37-68.

Dizayi, S. (2015). The crisis of identiy in post-colonial novel. *Proceedings of INTCESS15*-2nd International conference on education and social sciences: Instabul Turkey. Retrieved from www.reseachgate.net.

Flint, H. (1965). Zanzibar: 1890-1950. In V. HarlowandE. M. Chilver (Eds.), *History of East Africa* (Vol. II, pp. 647-649. Oxford: Clarendon press.

Furlong,A., Lovelace, A., & Lovelace (1999). *Basic reseach methods and statistics: An intergrated approach*. New York: Harcout college.

Gennep, A. (1960). *The rites of passage*. Chicago: University of Chicago press.

Glassman, J. (2011). *War of words, war of stones: Racial thought and violence in colonial Zanzibar*. Bloomington: Indiana University Press.

Gray, J. (1975). *History of Zanzibar: From the middle ages to 1856*. Conn: Greenwood press.

Haji, A. V. (2018). Kutathmini mbinu za usawiri wa wahusika katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Asali Chungu:* Utafiti linganishi. Tasinifu ya shahada ya umahiri katika Kiswahili (Haijachapishwa): Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Tanzania.

Haji, G. A. (2005). Upande wa pili wa riwaya teule za Shafi Adam Shafi: Dhamira zilizofichama. Tasnifu ya umahiri katika fasihi ya Kiswahili (haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania.

Ingrams, W. H. (1967). *Zanzibar: Its history and its people*. London: Frank Cass and company limited.

Kalua, A. F. (2007). The collapse of certainty: Contextualizing liminality in Botswana and Reportage. South Africa: University of South Africa.

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New age international publishing Ltd.

Kothari, C. R. (2009). Rese*rch methodogy: Methods and techiniques*. New Delhi: New age internationl publising Ltd.

Kyando, L. (2013). Majina sadfa ya wahusika katika *Kusadikika* na *Kichwamaji*. *Mulika*, 31, 37-50.

Lodhi, A. (1973). The institution of slavery in Zanzibar and Pemba. Research report No. 16. Uppsala, Sweden: The Scandinavian institute on African studies.

Lofchie, M. F. (1965). *Zanzibar: Background to revolution*. Princeton: Princeton university press.

Maurizi, V. (1984). *History of Seyyid Said, sultan of Muscat*. New York: The oleander press.

Mbogoni, L. (2018). *Miscegenation, identity and status in colonial Africa: Intimate Colonial encounters.* Taylor & Francis.

Mochiwa, Z. (2016, January, 21). Uchotara na ubaguzi wa Kizanzibari. Rai. Retrieved from www.pressreader.com.

Mohamed, M. S. (1978). *Nyota ya Rehema*. Nairobi: Oxford university press.

Mohamed, S. A. (1989). *Asali Chungu*. Nairobi: East Africa educational publishers.

Mohamed, S. A. (1947). *Dunia Mti Mkavu*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Mulokozi, M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Moccony printing press.

Mussa, F. K. (2007). *Mchango wa suala la ukombozi katika riwaya za Shafi A. Shafi*. Tasinifu katika shahada ya kwanza ya elimu na sanaa (Haijachapishwa): chuo kikuu cha taifa cha Zanzibar, Zanzibar.

Musyoki, C. Nd. (2016). Maudhui ya ubaguzi katika Mhanga wa Nafsi Yangu. Tasnifu ya umahiri ya idara ya Kiswahili, chuo kikuu cha Nairobi (haijachapishwa), Nairobi.

Ngaiza, M. K. (2003). Gender and political empowerment in the third millenium: A conceptual framework. *Tanzania journal of development studies*,4(1),167-212.

Oded, A. (2017). The Omani sultanate in Zanzibar and East Africa: Historical, political, economic and religious aspects. RIMA Historical Papers, Volume 5.

O'Reilly, C. (2001). *Post-colonial literature.* In A. Barlow (Ed.), *contexts in literature.* Edinburgh: Cambridge university press.

Pearce, F. B. (1920). *Zanzibar: The island metropolis of eastern Africa*. London: Smithsion institution libraries.

Ponera, A. S. (2019). Misingi ya utafiti wa kitaamuli na uandishi wa tasnifu. Dodoma-Tanzania: Central tanganyika press.

Prager, K. J. (2014). The dilemmas of intimacy: Conceptualization, assessment, and treatment. Washington, DC. APA.

Ricard, A. (2000). *Swahili thatre and individualism*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Robert, S. (1991). *Maisha yangu na baada ya miaka hamsini*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Romero, P. (2012). Seyyid Said bin Sultan bin Said of Oman and Zanzibar: Women in the life of this Arab patriarch. *British journal of middle eastern studies*, 39(3), 373-392.

Said, E. W. (1993). *Culture and imperialism*. New York: Vintage books.

Said, E. W. (1978). *Orientalism*. New York: Random house.

Said, A. S.( 2015). Matumizi ya ndoto katika riwaya za Kiswahili: Ulinganisho wa riwaya za Said Ahmed Mohamed na Mohammed Suleiman Mohamed. Tasnifu ya umahiri (Haijachapishwa): Chuo kikuu cha Dodoma, Tanzania.

Shafi, A. S. (1999). *Vuta N'kuvute*. Dar es Salaam: Mkuki na Nyota Publishers.

Shayo, M. K. (2011). Usawiri wa mimba za watoto wa nje ya ndoa katika riwaya: *Nyota ya Rehema* na *Vuta N'kuvute*. Tasnifu ya umahiri (Haijachapishwa): Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Tanzania.

Sheriff, A. (1987). *Slaves, spices and ivory in Zanzibar*. Athens: Ohio university press.

Sheriff, A. (2001). Race and class in the politics of Zanzibar. *Africa spectrum*, 36(3), 301-318.

Sigelman, L., & S. Welch (1994). Black Americans view of social inequality. Cambridge: Cambridge university press.

Thomassen, B. (2006). Liminality. In A. Harrington, B. Marshall and H.P. Müller (Eds.), *Routledge encyclopedia of social theory* (pp. 322-323). London: Routledge.

Thuranira, I. S. (2017). Maudhui ya ukoloni mambo leo katika tamthilia teule za Kiswahili. Tasnifu ya umahiri ya idara ya Kiswahili, chuo kikuu cha Nairobi (haijachapishwa), Nairobi.

Topan, F. (1971). *Mfalme Juha*. Dar es Salaam: Oxford university press.

Traore, F. (2008). Family and society in Said Ahmed Mohamed's novels. *Swahili Forum*, 15, 73-75.

TUKI (1981). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Dar es Salaam: Oxford university press.

Vernet, T. (2009). Slave trade and slavery on the Swahili coast (1500-1750). In B.A. Mirzai, I. M. Montanaet, P. Lovejoy. (Eds.), *Slavery, islam and diaspora* (pp. 37-76). Johannesburg: Africa world press.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi*: *Misingi na vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa.

Wa Thiong'o, N. (1977). *Petals of Blood*. London: Heinemann.

Young, R. (2001). *Postcolonialism: An historical introduction*. Oxford: Blackwell.

# VIAMBATANISHO

## Kiambatanisho namba Moja: Hatua za usomaji makini

Usomaji makini ndiyo mbinu iliyotumika katika kukusanya data za utafiti huu ambapo hatua kadhaa zilihusika. Hatua hizo ni:

Mosi: Hatua ya kwanza ilikuwa ni kusoma riwaya teule kwa ujumla wake ili kuweza kufahamu hasa kinachozungumzwa katika riwaya hizo.

Pili: Hatua ya pili ilikuwa ni kusoma kwa malengo ya kuanza kukusanya data kulingana na malengo mahususi ya utafiti. Hivyo mtafiti aliandaa shajara kwa ajili ya kudondoa sehemu ambazo zilikuwa ndani yake mna data za utafiti.

Tatu: Hatua ya tatu ilikuwa ni kudondoa data kutoka katika riwaya teule.

Nne: Hatua ya nne ilikuwa ni kuunganisha data kwa maana ya madondoo yanayofanana kuyaweka pamoja ili kuepuka uradidi wakati wa uchambuzi wa data.

Tano: Hatua ya tano ilikuwa ni kuchambua data kwa kuandaa mada ama vichwa kulingana na malengo mahususi ya utafiti.

**Kiambatanisho namba mbili: Muongozo wa uchambuzi wa data**

Data za utafiti zilichambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo ambapo hatua kadhaa zilifuatwa. Hatua hizo zilihusisha:

Mosi: Kupangilia data za utafiti kwa namna ambayo inakidhi matwakwa ama mahitaji ya malengo mahususi.

Pili: Kuchukuwa madondoo ya data za utafiti na kuyaweka kwenye kichwa ama mada husika.

Tatu: Kufanya uchambuzi wa data kwa kutoa maelezo ambayo yanajibu maswali ya utafiti.

Nne: Kuhusisha nadharia katika uchambuzi wa data.

Tano: Kufanya mjadala wa data za utafiti kwa kurejelea malengo mahususi ya utafiti.